# UBANIFU WA FANI KATIKA DIWANI YA *ALIDHANI KAPATA NA HADITHI NYINGINE*

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

NA

MUTUKU PERLICE NJERI

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2015

A1500674A
2015 theses

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.

Sahihi................................................. Tarehe...12.11.15...

Perlice N. Mutuku

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi

Sahihi................................................. Tarehe..12-11-15......

Dkt. Evans Mbuthia

Sahihi................................................. Tarehe...20/11/2015.

Dkt. Zaja Omboga

## TABARUKU

Kazi hii namtabarukia mume wangu Andrew Muthee na wanangu; Waithera, Muhoro, Mumbi na Levi ambao walionyesha uvumilivu mkubwa nilipoizamia kazi hii.

## SHUKRANI

Mwanzo namshukuru Mungu kwa kunipa siha njema tangu nilipozalika na kuniwezesha kukua na kukwea ngazi za elimu hadi kiwango hiki cha uzamili. Safari hii imekuwa ndefu na yenye panda shuka nyingi na uvumilivu. Imefanikishwa na kufikia kikomo kutokana na usaidizi wa watu wengi ambao sina budi kuwashukuru ingawa sitaweza kuwataja wote.

Shukrani zangu maalum nazitoa kwa wasimamizi wangu, Daktari Evans M. Mbuthia na Daktari Zaja Omboga kwa ushauri mawaidha na uelekezi wao. Nawashukuru wahadhiri wangu wote katika Idara ya lugha ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kunifunza, kunielekeza na kunipa moyo wa kuendelea na safari hii ndefu.Wao ni pamoja na Dkt. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Mwenda Mbatiah, Dkt. George Mweri, Dkt. Amiri Swaleh na Mwalimu Basillio Mungania.

Pia ningependa kumshukuru mume wangu, Andrew Muthee kwa kuwa changamoto katika usomi wangu, bila kumsahau Rev. Ezekiel Muendo kwa ushauri wake. Sitawasahau wanafunzi wenzangu tuliosaidiana nao kwa njia nyingi; si kwa nakala, si kwa mijadala na pia kwa namna tulivyotiana shime katika wakati mgumu. Wao ni: Kariuki Muriithi, Rose Shikenyi, Rono Jepng'etich, Lily Koech, Merolyne Otiende, Moraa Lydia na Florence Vutangwa.

# IKISIRI

Lengo la utafiti huu limekuwa kuchanganua ubanifu wa fani katika hadithi fupi katika diwani ya *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* (2011) iliyohaririwa na Iribemwangi. Mada imechaguliwa kwa misingi kuwa kazi ya kifasihi huzua maana kamili inapochunguzwa kimuundo na kifani. Aidha hadithi fupi zilizoteuliwa hazijawai kufanyiwa uhakiki wa kifani kwa mtazamo wa nadharia ya elimu mitindo. Utafiti wetu umelenga kuchunguza ubanifu katika usawiri wa wahusika na kubainisha nafasi ya matumizi ya lugha katika diwani husika. Nadharia ya elimu- mitindo imetumika katika uchanganuzi wa usawiri wa wahusika na uchambuzi wa kimtindo na imefaa utafiti huu kwa kutoa picha inayodhihirisha baadhi ya sifa za hadithi fupi za kimtindo na kifani kama zinavyodhihirika katika diwani ya *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine.*

Madhumuni yanayorejelewa yametumiwa kuunda maswali ya utafiti ambayo yametuongoza katika uchanganuzi wa usawiri wa wahusika na uchambuzi wa kimtindo katika diwani hii. Matumizi ya lugha katika diwani husika yamegunduliwa kusheheni methali, semi, tamathali za usemi, sentensi fupi, sentensi ndefu, dayolojia na monolojia. Matokeo ya utafiti yamebainisha kuwa matumizi ya lugha yamechangia dhamani ya kiujumi katika hadithi mahsusi na pia kuonyesha namna uhuru wa kutumia lugha katika uandishi huacha athari fulani iliyonuiwa. Utafiti huu pia ulidhihirisha kuwa wahusika katika diwani hii ni wahusika wa mraba mmoja.

## YALIYOMO

**Ukurasa**

Ungamo ....................................................................................ii

Tabaruku ....................................................................................iii

Shukrani....................................................................................iv

Ikisiri....................................................................................v

Yaliyomo....................................................................................vi

**Sura ya Kwanza** .................................................................... 1

1.0 Utangulizi....................................................................................1

1.1 Suala la utafiti....................................................................................3

1.2 Madhumuni ya utafiti....................................................................................4

1.3 Maswali ya utafiti....................................................................................4

1.4 Sababu za kuchagua mada ....................................................................................4

1.5 Upeo na mipaka ya utafiti....................................................................................5

1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada ....................................................................................5

1.7 Msingi wa kinadharia....................................................................................7

1.7.1 Nadharia ya Elimu Mitindo ....................................................................................7

1.8 Mbinu za utafiti....................................................................................9

**Sura ya Pili: Usawiri wa wahusika katika diwani ya *Alidhani Kapata na hadithi nyingine*....................................................................................**11

2.0 Utangulizi ....................................................................................11

2.1 Wahusika wakuu katika Diwani ya *Alidhani kapata na Hadithi Nyingine*....................12

2.1.1 Yakubu ....................................................................................13

2.1.2 Sista Yule ....................................................................................14

2.1.3 Beatrice....................................................................................15

2.1.4 Hamisi....................................................................................16

2.1.5 Sami....................................................................................16

2.1.6 Mtoro M'Mali....................................................................................17

2.1.7 Ndugire....................................................................................18

2.1.8 Binta....................................................................................19

2.2 Hitimisho ....................................................................................20

2.3 Wahusika wadogo katika Diwani ya *Alidhani kapata na Hadithi Nyingine*........... 20
2.3.1Hadithi ya Baisikeli........21
2.3.2 Hadithi ya Sista Yule........21
2.3.3 Hadithi ya Dakika za Adhama........23
2.3.4 Hadithi ya Shimo la Maisha........23
2.3.5 Hadithi ya Sami........24
2.3.6 Hadithi ya Namchukia babangu........25
2.3.7 Hadithi ya Fimbo ya Maradhi........25
2.3.8 Hadithi ya Achekaye Mwisho........26
2.4 Hitimisho........27
**Sura ya Tatu: Mtindo wa matumizi ya lugha katika diwani ya *Alidhani Kapata na hadithi nyingine*........29**
3.0 Utangulizi........29
3.1 Methali........31
3.2 Semi........32
3.3 Tamathali za usemi........33
3.3.1 Tashbihi........34
3.3.2 Sitiari........35
3.3.3 Tashihisi........36
3.3.4 Tasifida........38
3.3.5 Chuku........40
3.3.6 Maswali ya Balagha........41
3.3.7 Majazi........42
3.3.8 Tanakali za sauti........44
3.3.9 Mdokezo........45
3.3.10 Kuchanganya ndimi........46
3.3.11 Takriri........47
3.4 Sentensi fupi........48
3.5 Sentensi ndefu........49
3.6 Hitimisho........50

**Sura ya Nne: Matumizi ya dayolojia na monolojia katika diwani ya Alidhani Kapata na hadithi nyingine** ........52
4.0 Utangulizi........52
4.1 **Dayolojia** ........53
4.1.1 Dayolojia shawishi katika '*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine'*........54
4.1.2 Dayolojia ulizi katika'*Alidhani Kapata na HadithiNyingine'*........56
4.1.3 Dayolojia malumbano katika '*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine'* ......58
4.2 **Monolojia**........59
4.2.1 Monolojia katika 'Alidhani kapata' ........60
4.3 Hitimisho........64
**Sura ya Tano:** Muhtasari, Mahitimisho na Mapendekezo........ 66
5.0 Utangulizi........66
5.1 Muhtasari wa matokeo........66
5.2 Mapendekezo ya utafiti zaidi........68
Marejeleo........69

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Hadithi fupi ni hadithi inayojifunga kwa idadi ndogo ya wahusika na tukio fulani maalumu, isiyoonyesha mabadiliko makubwa ya matukio, mandhari au utanzu huu pia haujingizi kwenye undani wa wahusika. Mohamed (a995) alieleza kuwa hadithi fupi haina lazima kuchukua kila kipengele ambacho riwaya huchukua, na kama itachukua kipengele chochote, basi kitachukuliwa katika usahili wake. Pamoja na hayo, hadithi fupi ina vipengele vyake ambavyo kwa namna fulani vinajitofautisha na riwaya. Hadithi mara nyingi huchukua mkondo mmoja usiokuwa na matawi au vitawi vingi. Hakuna simulizi ambazo hazihusiani moja kwa moja na mwelekeo wa mkondo mkuu wa hadithi ambayo kwa kawaida inamhusu mhusika mmoja au inawahusu wachache.

Hadithi fupi ni kazi ya kubuni kwa kuwa masimulizi yenyewe huwa yanashabihiana na mambo yanavyokuwa katika maisha ya kila siku. Mwandishi wa hadithi fupi lazima azue kisa au tukio ili kulihadithia. Kulingana na Wamitila (2002), hadithi fupi ni utungo mfupi wa kinathari unaojishughulisha na suala fulani kuu, wenye wahusika ambao hawakuzwi kwa kina na unaotumia mbinu za kimaelezo za kiubanifu, zenye uelekezi wa kiwango cha juu. Utungo huu hautumii mandhari kwa upana na una athari kuu ya umoja. Utungo huu unaweza kusomwa kwenye kikao kimoja kifupi tu. Wamitila (2010) ameeleza kuwa hadithi fupi ni dhana inayotumiwa kuelezea utungo wa kinathari ambao unazungukia tukio moja kuu na unasimulia kisa kinachomhusu mhusika mmoja au wahusika wachache sana na unaozungumzia kipindi maalum kwa mtindo wa kibanifu.

Utanzu wa hadithi fupi umehusishwa kwa kiasi kikubwa na utanzu wa ngano katika fasihi simulizi. Katika fasihi simulizi, ngano ndio utanzu wenye uhusiano wa karibu sana na hadithi

fupi. Uhusiano huu unaonekana katika baadhi ya mikusanyiko ya hadithi fupi ambayo inajumlisha hadithi ambazo zina sifa za kingano. Ukuaji wa utanzu huu katika Fasihi andizi ya Kiswahili unaweza kusemekana kuwa umewekewa msingi na kuwepo kwa utanzu huu katika fasihi simulizi.

Tukio kuu linalojitokeza katika hadithi fupi haliwezi kudhihirika pasipokuwa na wahusika wanaoyatenda matukio hayo makuu. Waihiga na Kamau (2002) walisema kuwa katika kazi yoyote ya fasihi mwandishi hutumia wahusika kwa njia mbalimbali ili kuwasilisha ujumbe alionao. Mtunzi huongea na hadhira yake kupitia kwa wahusika aliowaumba. Waliendelea kusema kuwa mtunzi haongei kama afanyavyo mhubiri kanisani au kadhi msikitini, bali huwatumia wahusika wake kupitisha yaliyo moyoni mwake kwa wasomaji, watazamaji au wasikilizaji wa kazi yake. Kwa njia hii hadhira hupata ujumbe wa mwandishi kwa kuyachunguza yale wahusika wayasemayo, wayatendayo, waonekanavyo, wasemavyo na kila wakati wahusika hawa huwakilisha mtu au kundi la watu katika jamii.

Fani ni njia kuu ya kuwasilisha maudhui katika kazi ya fasihi. Wamitila (2010) anasema kwamba maudhui hayawezi kumfikia msomaji bila ya kuwepo kwa fani. Kimsingi, dhana hizi mbili hazipaswi kutenganishwa kwa kuwa fani si muhimu isipoangaliwa katika muktadha wa kile kinachowasilishwa na kinavyowasilishwa hasa kwa ubanifu wake katika hadithi fupi. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999), fani ni jumla ya nyenzo na mbinu zinazotumiwa na mwandishi ili aweze kuwasilisha maudhui yake. Fani ni dhana iliyo na vipengele kama vile wahusika, mtindo na usimulizi.

Kwa ufupi, fani ni jumla ya nyenzo zinazotumiwa kuzalisha maudhui na pia huhusu mbinu ambazo zinatumiwa katika lugha ili kuyaeleza yale mwandishi anayokusudia kuyaeleza. Kwa fani ni ufundi wa kisanaa. Ubanifu wa fani ni dhana inayotumiwa kutoa maelezo kuhusu jinsi

vipengele vya fani kama vile: wahusika, matumizi ya lugha, dayologia na monologia katika kazi ya kifasihi vilivyowasilishwa na msanii wa kazi fulani mahsusi. Katika uchunguzi huu, tutaangazia kipengele cha wahusika ambapo tutachunguza ubanifu wa wahusika katika usawiri wao, mbinu nyingine za matumizi ya lugha, dayolojia na monolojia.

## 1.1 Suala la Utafiti

Watafiti wengi wameshughulikia swala la fani katika tanzu tofauti hasa riwaya na tamthilia. Aghalabu inawezekana kuwa kutoshughulikiwa sana kwa fani katika hadithi fupi kunatokana na imani kuwa pengine fani haina uzito katika utanzu huu ikilinganishwa na tanzu nyingine. Katika ka mwanya kwa mfano ni mbayana kwa maswali ya fani ni ni changamano kutokana na ......yake mapana. Kwa hivyo si ajabu ya kwamba watafiti wengi wameshungulikia fani katika riwaya.

Diwani ya *'Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine'* tunayoihakiki ilichapishwa mnamo mwaka wa 2011. Katika uchunguzi wetu tumegundua kuwa kazi hii haijahakikiwa na mtaalamu yeyote hasa kuhusu ubanifu wa kifani, hivyo basi tumeamua kuhakiki namna wasanii hawa wamewasawiri wahusika na kutumia lugha kwa ubanifu ili kuwasilisha dhamira na mawazo yao. Kwa kuchanganua usawiri wa wahusika, matumizi ya lugha, dayologia na monologia katika diwani ya *Alidhani kapata na Hadithi Nyingine,* tumeliziba pengo hilo na kutoa mchango wetu wa kitaaluma.

## 1.2 Madhumuni ya Utafiti

Shabaha za utafiti ni:

i) Kuchunguza namna kipengele cha wahusika kilivyosawiriwa katika diwani ya *Alidhani kapata na Hadithi Nyingine.*

ii) Kuchunguza ubanifu wa matumizi ya lugha katika kuendeleza dhamira na maudhui katika diwani ya *Alidhani Kapata na Hadithi Nyinginezo.*

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti wetu umeongozwa na maswali yafuatayo:

i) Je, kipengele cha wahusika kimesawiriwa kwa njia ngani katika diwani ya *Alidhani kapata na Hadithi Nyingine?*

ii) Je, ubanifu wa matumizi ya lugha una nafasi gani katika kuendeleza maudhui na dhamira katika diwani ya *'Alidhani kapata na Hadithi Nyingine'?*

## 1.4 Sababu za kuchagua mada hii

Katika usomaji wetu, hatujapata ithibati yoyote ya kuonyesha kuwa kuna utafiti wowote uliowahi kufanywa kuhusu vipengele vya ubanifu wa kifani katika diwani ya *'Alidhani kapata na Hadithi Nyingine'* na kama upo sio mkubwa. Kwa hivyo utafiti wetu umejaribu iwezekanavyo kuliziba pengo hilo.

Usawiri wa wahusika katika utanzu wa hadithi fupi aghalabu umeshughulikiwa sana katika miongozo na tafiti za kawaida lakini sio kwa njia za kinadharia kama katika tanzu zingine za fasihi Andishi. Kwa hivyo Tunaamini kwamba utafiti huu umetoa mwanga wa kuhakiki wahusika na matumizi ya lugha katika utanzu huu kwanjia barabara.

## 1.5 Upeo na mipaka ya utafiti

Uchanganuzi wetu umejikita kwenye hadithi fupi za *`Alidhani kapata na Hadithi Nyingine`* (2011). Utafiti huu umehusu uchanganuzi wa vipengele vya ubanifu wa fani. Hata hivyo, palipotokea haja ya kutoa mifano zaidi, hatukuwa na budi kurejelea mifano kutoka katika hadithi fupi nyinginezo. Kwa kuwa vipengele vya fani ni vingi, utafiti wetu ulajikita katika uchanganuzi wa baadhi ya vipengele vifuatavyo wahusika, dayolojia, monolojia na mbinu nyingine za matumizi ya lugha. Tuliteua vipengele hivi kwa sababu vinahusiana na kujengana. Kwa hivyo uchanganuzi wetu ulimulika jinsi vipengele hivi vilivyobanwa katika kujenga kazi nzima.

Katika diwani ya *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* kuna hadithi kumi na nne. Katika uchanganuzi wetu tumeangazia namna ubanifu unavyodhihirika katika hadithi nane zifuatazo: 'Baiskeli', 'Sista Yule', 'Dakika za Adhama', 'Shimo la Maisha, 'Sami', 'Namchukia Babangu', 'Fimbo ya Maradhi' na Achekaye Mwisho'.

**1.6 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii**

Leech, G. na Short, M. (1981) katika Style *in Fiction* wameangalia mawanda tofauti ya mtindo. Pia, wamejadili kuhusu nadharia ya elimu- mitindo. Isitoshe, wameangazia kuhusu uhusiano wa mtindo na maudhui. Ingawa maelezo yao yalikuwa ya kijumla yalitufaa katika utafiti wetu.

Kibera (1988), alichunguza masuala katika hadithi fupi kwa njia wazi. Alijadili sifa za hadithi fupi kama vile urefu, wahusika, ploti, mandhari na maudhui. Pia alishughulikia sifa za muundo wa hadithi fupi. Maoni yake kuhusu wahusika yatakuwa ya manufaa katika utafiti huu.

Indangasi H. (1988) katika kitabu chake cha *Stylistics* amezungumzia masuala kadhaa ya elimu mtindo. Amezungumzia historia ya elimu-mitindo na viwango vya kuchunguza mtindo kama vile fonolojia, semantiki, sintaksia, msamiati na tamathali za usemi. Uchanganuzi huu umetupatia mwelekeo mzuri wa kuchambua kazi yetu ya uchambuzi wa kimtindo katika diwani ya *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*

Msokile (1993), ameeleza wahusika kama kigezo kikuu katika uundaji wa kazi ya sanaa. Msokile. Msokile ameshauri wahusika kwa kuchunguza wema na ubaya. Wahusika waliomo katika makundi haya huwakilisha tabia maalumu inayotaranjiwa katika jamii. Kazi hii ilitufaa katika utafiti wetu kwa sababu dhana aliyoizungumzia ya 'wema' na 'ubaya' imetusaidia kwa uchanganuzi wa wahusika kwa sababu utafiti wetu umezama katika kuchanganua wahusika, uhusika wao na namna wanavyojieleza kwa, monolojia na dayolojia

Naye Mohochi (1995), alichanganua vipengele vinne vya fani ambavyo ni: wahusika, ploti, lugha na usimulizi. Alihakiki hadithi nne za waandishi tofauti. Kazi hii yake ni muhimu kwetu kwa sababu inaangazia kipengele cha fani ya wahusika ambayo ndiyo tumeishughulikia katika utafiti wetu huu.

Mohamed (1995), ameangazia mbinu za kumfahamu mhusika tokea mwanzo na kuweza kumfuata mhusika huyo kwa urahisi. Aidha ametoa mbinu ya kumwangazia mhusika hasa tabia yake, kutokana na yale anayoyatenda au anayotendewa au anayotendana na wahusika wengine wenzake au hata kutokana na maneno yake. Kazi hii imetufaa zaidi katika kazi yetu kwa sababu itatuelekeza katika kuchanganua wahusika, uhusika wao, dayolojia na monolojia.

Katika kazi yake Ndung`u (1996), alishughulikia fani katika riwaya za Katama Mkangi. Kazi hii imetufaa katika utafiti wetu hasa kwa kurejelea vipengele vya fani alivyochanganua ingawa utafiti wetu umekuwa unarejelea fani ya wahusika katika hadithi fupi wala si riwaya.

Mwangi (2005), aliangazia kipengele cha fani katika tamthilia za Wamitila. Alishughulikia ploti katika kazi hizi, umbuji wa wahusika na matumizi ya lugha. Kazi hii imekuwa ya manufaa kwetu kwa kuwa utafiti wetu umeangazia vipengele vya wahusika, dayolojia na monolojia, lakini tofauti na Mwangi tumerejelea hadithi fupi za 'Alidhani kapata na hadithi nyingine'.

Mbuthia (2005), amehakiki kipengele cha mtindo na maudhui kwa kina. Amechanganua diwani kumi na nne za Kiswahili kuanzia zile za awali hadi zile za hivi karibuni. Kazi hii imekuwa ya manufaa kwetu kwa sababu ameangazia kipengele cha mtindo ambacho pia kimeshghulikiwa katika kazi yetu.

Wamitila (2010), anaeleza kuwa uendelezaji wa wahusika, undani wa kisaikolojia na ukuaji wao unajitokeza vyema katika tanzu ambazo ni ndefu. Kwa hivyo mwandishi wa hadithi fupi hulazimika kutumia mbinu ambazo ni muhimu katika kuiendeleza dhamira, mfano mihusianisho (analojia) ambayo inamwezesha msomaji kumwelewa mhusika kwa misingi ya ulinganishi ambao unadokezewa na sifa za mhusika huyo.

## 1.7 Msingi wa Kinadharia

Kazi hii itategemezwa nadharia ya elimu-mitindo

### 1.7.1 Nadharia ya Elimu Mitindo

Uchunguzi wa nadharia ya elimu mitindo katika karne ya ishirini ulibadilisha na kupanua uchunguzi wa awali wa ufasaha katika usemaji. Mnamo mwaka wa 1909, shauku katika elimu mitindo ilianza kuenea polepole katika Bara la Ulaya. Katika miaka ya 1960, ndipo uchunguzi wa elimu mitindo ulistawi nchini Uingereza na Marekani kutokana na msukumo wa maendeleo baada ya Vita Vya Pili vya Dunia.

Nadharia tutakayoitumia katika utafiti wetu kuchanganua ubanifu wa fani katika Diwani ya *Alidhani Kapata* na *Hadithi Nyingine* ni Elimu-Mitindo. Leech na Short (1981) wanaeleza kuwa elimu-mitindo ni uchunguzi wa mtindo. Aidha wanaendelea kueleza kuwa mtindo ni namna lugha inavyotumiwa katika muktadha na mhusika fulani kwa lengo maalumu. Zaidi wanatilia mkazo kuwa neno mtindo katika upana wake linatumika kwa usemi wa kimazungumzo na maandishi katika masuala ya kifasihi na yasiyo ya kifasihi. Kwa namna nyingi, elimu mitindo inakaribiana sana na uhakiki wa kifasihi au uhakiki wa kiutendaji. Mara nyingi kazi inayochunguzwa ni ya kifasihi na msisitizo huwekwa kwenye matini. Lengo la uchunguzi wa kimtindo sio kuelezea sifa za matini tu bali ni kuonyesha uamilifu na umuhimu wake katika kufasili matini yake.

Nadharia ya elimu mitindo wakati mwingine hukanganya kwa kuitwa elimu mitindo ya kifasihi au elimu mitindo ya kiisimu. Inaitwa elimu mitindo ya kifasihi kwa sababu inaangazia matini za kifasihi. Kwa upande mwingine inaitwa elimu mitindi ya kiisimu kwa sababu zana zake muhimu huchotwa tutoka kwa isimu. Hata hivyo elimu mitindo ya kiisimu

inatumiwa kurejelea aina ya mtindo ambao lengo lake sio tu matini za kifasihi, lakini hata hutumika kwa uchunguzi wa kiisimu. Elimu mitindo inaweza kutumika kama dhana ya kijumla ambayo inahusu uchanganuzi wa lugha anuwai.

Indaghasi, H. (1988) anaeleza kwa uwazi uamili wa elimu mitindo. Anasema kwamba elimu mitindo imesaidia kuondoa maoni ya wahakiki yasiyo na msingi kuhusu kazi za kifasihi na hasa kuhusu lugha za kazi hizo. Vile vile, elimu mitindo imesaidia kuondoa utata uliokuwapo kati ya fani na maudhui kwa kutoa maelezo ya lugha ya kifasihi kama kitu kinachoweza kutabirika. Aidha, elimu mitindo hutupatia mbinu za kuchanganua upekee wa kazi za kifasihi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), elimu-mitindo ni dhana inayotumiwa kurejelea taaluma inayohusu uchunguzi wa jinsi mbalimbali za kueleza matukio katika kazi za kifasihi. Ni taaluma inayochunguza jinsi lugha inavyojidhihirisha katika matini ya kifasihi na yasiyo ya kifasihi.

Nadharia ya elimu-mitindo ni nadharia ambayo ni changamano. Ina uwezo wa kuchanganua maswala ya kifasihi na kiisimu. Tumeamua kuitumia kwa sababu ina uwezo wa kushughulikia ubanifu wa wahusika, matumizi ya lugha, dayolojia na monolojia katika diwani ya '*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine.*' Katika utafiti wetu tumetumia mtazamo wa elimu-mitindo ya kifasihi kwa sababu zana zake muhimu huchotwa kutoka kwa fasihi. Elimu-mitindo inaweza kutumika kama dhana ya kijumla ambayo inahusu uchanganuzi wa lugha anuwai zisizo za kifasihi au sajili mbali mbali. Kwa sababu ya upeo huo mpana, elimu-mitindo inakaribiana sana na mitazamo ya ki- isimu jamii.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

Utafiti wetu umekuwa wa maktabani. Tumesoma hadithi zote katika diwani ya *'Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine'* (2011). Katika usomaji wetu tumefanya juhudi za kutambua zile hadithi ambazo zimeshamiri sifa nyingi zinazotambulisha utanzu wa hadithi fupi na kubainisha ubanifu wa kifani katika vipengele tulivyoviteua. Hadithi zilizochaguliwa ni: 'Baisikeli' na Karuru, 'Sista Yule' na Fauzia, 'Dakika za Adhama' na Ngugi wa Thiong'o, 'Shimo la Maisha' na Raya Timmamy, 'Sami' na Mwenda Mbatia, 'Namchukia Babangu' na Iribemwangi, 'Fimbo ya Maradhi' na Sam Ng'ang'a na 'Achekaye Mwisho' na Iribemwangi.

Tumejikita katika uchunguzi wa baadhi ya vipengele vya fani na ubanifu wake na namna wahusika walivyosawiriwa, matumizi ya lugha, dayolojia na monolojia. Aidha tumesoma vitabu, majarida, tasnifu na makala ya waandishi wengine ambayo yana uhusiano na mada tunayoitalii. Pia tulisoma kazi zinazohusiana na nadharia ya Elimu-Mitindo pamoja na zile zinazogusia kipengele cha fani. Maandishi haya yametufaa katika kuifahamu nadharia na vipengele vya ubanifu wa fani na hivyo kutuwezesha kutumia nadharia hii ya uhakiki ipasavyo na kuchanganua ubanifu wa fani kwa njia mwafaka.

Isitoshe wataalam na wasomi wa Kiswahili walitufaa sana kutokana na maoni na mijadala yao kuhusu mada hii. Mawazo yao yamekuwa ya manufaa katika utafiti wetu. Kisha tulichanganua data tuliyoikusanya na kuiwasilisha kwa mbinu ya kiuelezi.

# SURA YA PILI

# USAWIRI WA WAHUSIKA KATIKA DIWANI YA *ALIDHANI KAPATA NA HADITHI NYINGINE*

## 2.0. Utangulizi

Matukio yote katika hadithi hudhihirika kutokana na Maneno na matendo ya wahusika. Waihiga na Kamau (2002) walisema kuwa katika kazi yoyote ya kifasihi, mwandishi hutumia wahusika kwa njia mbalimbali ili kuwasilisha ujumbe alionao. Mtunzi huongea na hadhira yake kupitia kwa wahusika aliowaumba. Aidha mtunzi haongei kama afanyavyo mhubiri kanisani au kadhi msikitini, bali huwatumia wahusika wake kupitisha yaliyo moyoni mwake kwa wasomaji, watazamaji au wasikilizaji wa kazi yake. Kwa njia hii, hadhira hupata ujumbe wa mwandishi kwa kuyachunguza yale wahusika wayasemayo na wayatendayo. Kila wakati, wahusika hawa huwakilisha mtu au kundi la watu katika jamii. Katika uchanganuzi wetu katika diwani ya *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* tumeangazia aina mbili kuu za wahusika nazo ni: wahusika wakuu na wahusika wadogo.

Wahusika ni sehemu ya fani. Wahusika ni viumbe wa mawazoni mwa mtunzi ambao hutumiwa kuwasilisha mawazo ya mwandishi kwa hadhira. Kwa hivyo, wahusika ni wakala wa mtunzi kwa hadhira yake. Njogu na Chimerah (1999) walieleza kuwa wahusika ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Msanii huwaweka wahusika wake katika mandhari yatakayomsaidia kuwasilisha hoja zake kutokana na vitendo, maingiliano na tabia zao. Wahusika wanaweza kuwa binadamu, wanyama, wadudu na pia vitu visivyo na uhai. Hivyo wahusika ni viumbe wa hadithini wanaotokana na mawazo ya mwandishi na wanaoumbwa ili kuwasilisha ujumbe wa mwandishi

Wahusika wakuu wa hadithi fupi hawakuzwi sana na husafiri mawanda mafupi. Wahusika wakuu wa hadithi fupi huhusika katika kazi yote ya mwandishi na migogoro mikuu huwazunguka wao. Aidha wahusika wakuu katika utanzu huu hawabadiliki katika mawazo na matendo yao, na hudhihirisha msimamo dhabiti katika mawazo na matendo yao. Wahusika wadogo hawachukui nafasi kubwa katika hadith fupi. Hutumiwa kujenga na kukuza dhamira fulani maalum.Wahusika hawa huwa na mchango fulani kwenye dhamira kuu lakini nafasi yao inabaki ndogo na hawaelezewi sana katika hadithi fupi. Sifa ya ubanifu wa fani unaodhihirika katika diwani ya '*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*' kutokana na jinsiwahusika walivyosahukika.

### 2.1.0 Wahusika Wakuu.

Hawa ndio nguzo ya kazi yoyote ya kifasihi na ndio wanaosheheni hadithi nzima. Huisukuma hadithi mbele kwa sababu matendo na migogoro yote muhimu inawahusu. Dhamira kuu ya mwandishi hujitokeza kupitia kwao. Muingiliano wao na wahusika wengine ndio mbinu inayotumiwa kufafanua dhamira kuu.

Katika uchanganuzi wetu wa jinsi wahusika wakuu walivyobanwa, tumeangazia wahusika wakuu katika hadithi nane. Nao ni: Yakubu katika 'Baisikeli', Sista Yule katika 'Sista Yule', Beatrice Wanjiru katika 'Dakika za Adhama' Hamisi katika 'Shimo la Maisha', Sami katika 'Sami', Mtoro M'mali katika 'Namchukia Babangu', Ndugire katika 'Fimbo ya Maradhi' na Binta katika 'Achekaye Mwisho'.

### 2.1.1. Yakubu

Katika hadithi ya Baiskeli Yakubu ni mwanamme wa umri wa makamo Mungu atamtoa katika shida. Anakabiliwa na pandashuka za maisha lakini mwishowe anabahatika kupata Baiskeli. Katika hadithi hii, Yakubu anajitoketza kamani mcha Mungu. Ana imani kwamba Mungu atamtoa katika shida. anaa na kndelezaana ushiriki mawazo makuu ya mwandishi katika hadithi hii. Amepewa majukumu kadha na mwandishi yanayosaidia hadhira kumwelewa zaidi mhusika huyu.Yakubu amepewa jukumu la kukidhi mahitaji ya jamii yake iliyoishi katika uhitaji mkubwa.

Yakubu anawajibika kujitetea katika hali ngumu na kudhihirisha usemi kuwa "Akili ni nywele kila mtu ana zake." Kutokana na hali na mazingira aliyoishi, Yakubu alipata uelewa wa maisha kuhusu jinsi ya kujinasua kutokana na mitego migumu ya maisha.Wakati alihisi njaa alikula githeri cha shillingi kumi, alitembea mguu kila asubuhi hadi kazini kwa sababu hangeimudu nauli ya kwenda na kurudi jioni kutoka kazini

Pia Yakubu amesawiriwa kama mhusika anayetumia ujanja ili kutimiza kilio cha moyo wake. Alipowekelewa na askari kosa la kuendesha baiskeli isiyo na taa(na hakumiliki baiskeli) kwa ujanja alikiri kosa lake na kumuomba hakimu aonewe hisani na kurudishiwa baiskeli. Hakimu aliamrisha arudishiwe baiskeli yake! Yakubu amesawiriwa kama mhusika mwenye bidii katika kazi yake. Alikoajiriwa katika kampuni ya Nerak Top Flowers alifanya kazi chungu nzima bila kujali hali ya anga. Alikuwa akibeba pampu ya lita ishirini iliyoning'inia mabegani mwake tangu asubuhi hadi jioni.

Mhusika huyu amesawiriwa kama mcha Mungu. Baada ya kutoka kazini kila Jumatano alipitia kanisani ili kushiriki na wenzake katika maombi kwa kuwa hakukuwa na jambo

lingine lililompa amani na utulivu maishani kama ushirika wa maombi, mahubiri na nyimbo usawiri wa umebanwa Yakubu amebanwa na mwandishi. Kwa kuwa mengi kumhusu hayajasimuliwa.

Yakubu anadhihirika kuwa mhusika wa mraba mmoja. Habadiliki hata hali ya mazingira yanapobadilika. Ana imani na msimamo dhabiti katika namna anavyoendesha shughuli zake. Kwa mfano wasomaji hawaekezwi asiliyake. Wanakumbana naye katika hali ya umaskini.

### 2.1.2 Sista Yule

Hadithi hii inaeleza juu ya sista wa kidini aliye na mwenendo kinzani kando na yanayotarajiwa. Sista yule ni mhusika wa kike katika hadithi ya "Sista Yule" ya Fauzia, J. Kavishe. Amepewa majukumu makuu katika hadithi hii. Migogoro mikuu inamzunguka yeye. Anajitwika jukumu la kuhubiri neno la Mungu kwa watu wengine huku akitetea haki za watu lakini kusudi lake ni kuiba.

Unafiki wake unampelekea kujifanya kuwapenda watoto. Anaposafiri katika gari la umma anamhadaa mama mmoja kwa kumbeba mtoto na kumpa pipi huku akiilenga simu yake aina ya "Samsung". Sista Yule pia amesawiriwa kama mwizi anayetumia dini kuficha uovu wake. Anapowakuta Bakari na Juma mle kibandani anawaeleza juu ya injili huku macho yake amekaza kwenye simu ya"Samsung *660" ya yule mama.

Licha ya jina la kimajazi alilopewa, tabia yake haiafikiani na jina na mavazi yake.Yamkini jina hili ni la kitashtiti. Mwandishi amemuelekeza kwa lengo maalum la kudhihirisha ukinzani wa matarajio na maadili ya kijamii. Hatimaye hila zake zilipogunduliwa watu wengi walishanganzwa na unafiki wake. Sista Yule amebanwa kwa kuelezwa upande mmoja tu.

Hatuwelezwi asili yake.msomaji haelezwi kuingilia wizi pia msomaji hapata kujua kama ameolewa au la au kamaana watoto.

**2.1.3 Beatrice.**

Ni mwanamke afanyaye kazi katika kilabu. Jambo alifanyalo pasina matarajio yake. Amepitia mateso ya kisaikolojia jambo linalompelekea kuwa mwizi. Beatrice Wanjiru ni mhusika mkuu katika hadithi 'Dakika za Adhama' ya Ngugi wa Thiong'o. Ni mhusika msichana aliyefanya kazi ya kuuza vilabuni. Alikuwa kama ndege aliyejeruhiwa kwa kukosa wateja katika kazi yake, jambo lililomfanya kuhamahama kutoka klabu kimoja hadi kingine. Amesawiriwa kama mhusika asiyewavutia watu. Katika kilabu alikofanya kazi Wenzake waliweza kuwavutia wateja kwa urahisi jambo ambalo hakuliweza.Wateja wengi walimpuuza jambo ambalo lilimfanya kuwaonea Wenzake uivu. Mwandishi anamueleza kutokana na mtazamo huu mmoja pekee, hatupati kujua sifa zake nyingine.

Ametumiwa kujenga picha ya umasikini kwa kukaa kwa muda bila kazi. Alipata ajira kule Ilmoru katika baa ya Tree Tops Lodging and Restaurant, ambapo kama mwajiriwa, Beatrice alipata kujuana na mzee mwenye lori la magurudumu kumi na mawili .Alifanya urafiki naye na akafanikiwa kumhadaa na kumwibia pesa nyingi. Beatrice ni mhusika bapa anayependa anasa toka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Alitamani mapenzi kutoka kwa wanaume pale vilabuni. Kutokana na shauku hii alimuonea gere mwenzake Nyaguthii ambaye alikuwa mpinzani wake.Daima alifanya juhudi za kujirembesha ili awe na mvuto kwa wateja wa vilabu vya pombe.

**2.1.4 Hamisi**

Katika hadithi ya "Mashimoni" Hamisi na dadake ni mayatima wanaoishi katika umaskini mkuu. Ni mwanafunzi wa chuo kikuu na mwenye aliye na bidii sana. Yeye ndiye mhusika

mkuu katika hadithi ya "Shimo la maisha" na Dkt. Rawaya Timammy. Ni kijana mvulana aliye yatima aliyelelewa katika umasikini uliokithiri kule Kibera katika mtaa wa Mashimoni. Kutokana na hali ya maisha aliyoishi yeye na dadake. Alilazimika kufanya kazi ya vibarua ili aweze kupata kujikimu. Pia alivaa nguo zilizoraruka. Amesawiriwa kama mhusika aliyekumbana na shida nyingi za kimwili na kisaikolojia. na hata njaa. Mambo haya yalichangia kuzorota kwa afya yake. Alilazimika kufanya kazi kwa bidii ili aweze kujimudu na pia kumsaidia dada yake aliyekuwa mwanafunzi wa shule ya msingi ilhali alikuwa mwanafunzi wa chuo kikuu.

Ni mhusika aliye na uvumilivu na tumaini katika maisha. Hata baada ya dadake kuaga, na yeye kuanguka mtihani alikuwa na matumaini maishani. Amesawiriwa Kama mhusika mwenye bidii afanyaye kazi kwa kujitolea bila kufa moyo. Hamisi amesawiriwa na mwaandishi kama muhusika aliye na sifa ya uvumilivu katika maisha. Toka mwanzo hadi mwisho wa hadithi ya 'mashimoni' Hamisi amechorwa kama mhusika wa mraba mmoja asiyebadilika hata hali inapobadilika. Kwa hivyo ni mhusika bapa anayeshikilia msimamo dhabiti kwenye hadithi. Kutoka na ukweli kuwa ni muhisika bapa uhusika wake unabanwa kwa kuwa hawezi.

### 2.1.5 Sami

Katika hadithi ya "Sami" Sami amezungukwa na matatizo mengi ya kiafya, kiuchumi na kimaisha kwa jumla. Licha ya panda shuka hizi anajipa moyo. Katika hadithi ya "sami", Sami ni mhusika mvulana, mtotowe Baba Sami na Mama Sami. Aliishi katika mtaa wa Majengo. Amepewa jukumu la kuongoza kikundi cha WAMA (Wanamazingira wa Majengo) Sami ni mwasisi wa kikundi cha WAMA na wanachama walikuwa na imani naye na kumheshimu sana

Babake alimshawishi apate mpenzi kama vijana wengine kule majengo. Ushauri huu ulimletea maafa kwa sababu alipojiingiza. Kwenye anasa alipatwa na ugonjwa wa ukimwi. Sami ana msimamo na uamuzi dhabiti. Baada ya kutibiwa bila kupata afueni aliamua kwenda kituoni kupimwa. Alipata dawa na baada ya muda alianza kupata afueni. Sami anadhihirika kuwa mhusika bapa. Ni hodari licha ya hali yake ya afya. Anajikakamua kujua jinsi wenzake wanavyonawiri katika maisha. Habadiliki hata baada ya afya yake kuzorota. Mhusika huyu ni mwema tokea mwanzo mpaka mwisho.

Uhusika wake umebanwa kwa kuwa .......sana pengine kama ungalikuwa

### 2.1.6 Mtoro M'mali

Hadithi hii inarejelea maisha ya Mkata Mmali pamoja na jamii yake. Ukatili wake ndio aliosababisha maafa yaliyoikumba familia yake. Ni mwanawe mzee M'mali aliyepewa jukumu la usimulizi katika hadithi 'Namchukia babangu' ambapo mwandishi ametumia usimulizi wa nafsi ya kwanza. Amepewa jukumu la kuweka bayana masaibu yaliyoikumba familia ya mzee Mkata M'mali. Mwandishi anatueleza kuhusu Kifo cha kakake Mafutu kutoroka kwake kutoka nyumbani, kifo cha mamake, kutanda kwa wingu la ugonjwa na chanzo cha ugonjwa ulioimaliza familia ya Mzee Mkata M'mali.

Amesawiriwa kama mhusika mwenye kinyongo; asiye na moyo wa kusamehe. Anaeleza kuwa anamchukia babake sana kuliko chochote duniani. Hakutishwa na hali ilivyokuwa nyumbani kwao. Ndiye aliyewanusuru nduguze kutoka kwa utumwa wa baba yao nyumbani. Ni mhusika mwenye maono na bidii kwa sababu alipotorokea kule mjini alijiendeleza kimasomo na kuwa mhandisi. Aliweza kupata kazi na shirika la National Water Authority na

baadaye kuajiriwa na shirika la kimataifa kama mhandisi mkuu wa kanda ya Afrika Mashariki na Kati.

Mtoro M'mali ana msimamo wa dhati toka mwanzo hadi mwisho. Amesawiriwa kama anayemchukia babake tangu mwanzo, na hadithi inahitimishwa akiiendeleza chuki hiyo. Kwa hivyo, Mtoro M'mali ni mhusika bapa. Mwandishi amembana katika matukio mahususi yanayoakisi sifa za hadithi fupi.

### 2.1.7 Ndugire

Ni mhusika mkuu katika hadithi ya 'Fimbo ya Maradhi'. Ni mumewe Nyokabi na mtoto wa Thuo na Njoki. Anatafuta ushauri kutoka kwa babake wakati anahisi kukosewa na mkewe. Utaratibu wa kumrudisha Nyokabi alipotoka kwake ulikuwa mikononi mwa babake na wazee wasiopungua watatu. Ni mtiifu kwa ushauri wa wakubwa wake. Babake Thuo alimshauri kuwa ampe wakati aweze kutafiti kuhusu jambo lililokuwa na utata. Alitii maagizo ya mzee mponyaji ya kulala chali na kuwekelewa ini la kondoo mradi apate suluhu kwa shida iliyomkabili.

Ni mwigizaji. Baada ya babake Thuo kutoka kwa Mugo mzee Mponyaji, alimweleza jinsi atakavyojifanya ili aweze kung'amua ukweli. Alihitajika kutoamka asubuhi kwa kujifanya mgonjwa ili waweze kuona jinsi mkewe atakavyomshughulikia. Na mzee Mponyaji aliposema 'kauli ya mizimu haikatiwi rufani' Ndugire aliigiza kitendo cha kutapatapa kama anayekata roho.

Ndugire ni mhusika bapa. Hii ni kwa sababu anaamini anayoambiwa na babake na kuamini kuwa yana manufaa kwake. Alipoambiwa na babake na yule mzee Mponyaji aigize jambo fulani, alikubali na kuliigiza.

### 2.1.8 Binta

Binta ni mhusika mkuu katika hadithi ya 'Achekaye Mwisho 'ya ribemwangi. Ni msichana wa umri wa makamo ambaye amesoma masomo ya kiwango cha juu. Tayari ana shahada za B.Com na MBA. Aidha amefuzu katika taaluma ya uhasibu na ana cheti cha CPA na CK. Amelelewa katika mazingira ya utajiri. Alisoma Bran School kabla ya kwenda London na hatimaye California, Los Angeles. Ni msichana tajiri na aliye na mapenzi kwa wanaume. Ameimarika kiuchumi na ni mweka hazina wa chama cha wahasibu mjini.

Ni mhusika mwenye kiwewe na wasiwasi. Alipokua na shauku kukutana na Dennis Kitsakitsa. Ijapokuwa alipokuwa na kazi nyingi mle ofisini, alitanzama mishale ya saa kila mara huku akihisi ya kwamba muda hausongi.

Ni mwenye kutosheka na kuridhika kwa haraka na kufanya uamuzi wa haraka. Fedha zilipokuwa nyingi alikosa hamu ya kufanya kazi ya kuajiriwa na akaandika barua ya kujiuzulu.

Ni mjeuri na mwenye matusi. Haambiliki hasemezeki. Bwanake alipomshawishi wamwone daktari ili waweze kubaini kilichosababisha wao kukosa mtoto. Badala ya kuzingatia ushauri wake alimrushia mumewe matusi na kutaka apewe talaka.

Mhusika huyu ni tofauti na wahusika wengi wa hadithi fupi anabadilisha misimamo yake mara kadhaa. Hii ni kwa sababu anabadilikabadilika na hana msimamo dhabiti. Ndiye aliyemtaka Kitsakitsa kwenye uwanja wa ndege, lakini akawa ndiye wa kumgeuka na kumtaka talaka. Pia baada ya kufanya kazi kama muajiriwa na kupata pesa alikuwa anaomba kazi ya kuajiriwa, lakini akipata pesa nyingi aliandika barua ya kujiuzulu kwa nia ya kufanya kazi ya kibinafsi. Hivyo hana msimamo dhabiti. Huyu ni miongoni mwa wahusika wachache katika utanzu wa Hadithi fupi ambao hubadilisha mielekeo yao. Ingawaje amebanwa kama muhusika, ambanwa kama wahusika wengine katika diwani hii.

## 2.3 Hitimisho

Wahusika wakuu wamebanwa katika mtazamo mmoja katika usawili wao. Wamedhihirisha hali hii kwa kudhihirika kuwa wahusika. Kila mhusika mkuu katika hadithi zilizoteuliwa amesawiriwa kama mhusika aliye wa mraba mmoja asiyebadilika hata hali na mazingira yanapobadilika.

## 2.4 Wahusika wadogo

Hawa ni wahusika ambao hawachukui nafasi kubwa katika kazi bali hutumiwa kukuza dhamira kuu pamoja na kumjenga mhusika mkuu. Wahusika hawa wanatumiwa ili kumsaidia msomaji kumwelewa vyema mhusika mkuu. Kupitia maingiliano baina ya mhusika mkuu na wahusika wadogo tunapata mwanga zaidi kuhusu hulka ya mhusika mkuu.

Uchanganuzi wetu wa wahusika wadogo utamulika wahusika katika kila hadithi tuliyochagua kushughulikia kwenye sura hii yetu. Hadithi hizo ni kama vile; 'Baisikeli 'ya D.W. Karuru, 'Sista Yule' ya Fauzia, 'Dakika za Adhama' ya Ngugi wa Thiong'o, 'Shimo la Maisha' ya

Raya Timmamy, 'Sami' ya Mwenda Mbatia, 'Namchukia Babangu' ya Iribemwangi, 'Fimbo ya Maradhi' ya Sam Ng'ang'a ' ya Achekaye Mwisho' na Iribemwangi.

### 2.4.1 Wahusika wadogo katika hadithi ya 'Baisikeli'

Katika hadithi ya 'Baisikeli', wahusika wadogo ni kama vile; Askari Mrefu na Askari Mfupi, Hakimu, Sarai, Mzee, mwanamke mjamzito na watoto wake tisa.

Askari mrefu na Askari mfupi ni maafisa wa polisi waliopewa jukumu la kulinda usalama wa watu na kuwafungulia mashtaka wahalifu. Kwa nyumba ni wahusika wenye ari ya kazi. Wamesawiriwa kama wahusika wanaopokea hongo kutoka kwa raia na wasipofanikiwa katika maovu haya wanawatia raia matatani kwa kuwasingizia makosa. Wahusika hawa ni bapa katika msingi ya kuwa wanadhihirisha uovu tangu mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Wanajifanya wantii amri na wanaowahudumia watu kufuatana na sheria ilhali wanaitisha hongo na kuwalimbikizia mashtaka ya uongo kila wakikosa kutoa hongo.

Naye hakimu amepewa jukumu la kuwahukumu wahalifu kortini. Amesawiriwa kama mhusika mwenye utu. Yakubu anapoomba korti imuonee hisani, anakubali. Ni mwenye kutoa amri isiyokiukwa na inayopaswa kutekelezwa vivyo hivyo. Hivyo ni mhusika bapa.

Sarai, Mzee, mwanamke mjamzito na watoto tisa ni wahusika ambao hawajapewa majukumu makubwa. Sarai ni mkewe Yakubu. Mzee na mwanamke mja mzito ni baadhi ya watu walioshikwa kwenye msako. Watoto tisa ni watoto wake mzee Yakubu.

### 2.4.2 Wahusika wadogo katika hadithi ya "Sista Yule"

Katika hadithi ya 'Sista Yule' ya Fauzia, wahusika wadogo ni; utingo, abiria, mama mtoto, mzee, Bakari, James, Jumà, sugusugu, vijana na rasta.

Bakari, James na Juma wamepewa majukumu mahususi, kwamba wote ni wanabiashara katika mtaa wa Tengeru wanakouza nguo za mitumba. Wamepewa jukumu la kutatua kosa la jinai. Wanahusika kwa kuunda njama ya kumnasa mwizi wa simu pale Sonawari. Wanamuokoa mama mwizi anapoinyakua begi na kutimua mbio. Ni wahusika waadilifu licha ya wao kuwa na shughuli nyingi za kikazi, wanapanga mikakati ya kukomesha wizi katika maeneo ya mtaa wa Tengeru na Sonawari. Walijali maslahi ya watu wengine kwa kukomesha uovu uliokuwa umekithiri katika mtaa wa Tengeru.

Mama mtoto ni mwathiriwa wa wizi katika kituo cha magari cha Sonawari. Ni mhusika aliye na ushirikiano mwema. Alishirikiana na Bakari, Juma na sugusugu wa pale Sonawari kumnasa mwizi. Rasta ni mhusika wa kiume aliyekuwa mwizi pale vibandani eneo la Tengeru. Ni mtotowe mzee Lowasa ambaye alikua amejiweka. Ni kinyume cha babake ki-tabia.

Sugusugu ni walinzi waliopewa jukumu la kudhibiti tabia njema katika sehemu ya Tengeru ns Sonawari. Baada ya kujulishwa kwa simu wawe tayari pale stesheni ya Sonawari, walisaidia katika upekuzi wa abiria ambapo simu zilizopotea ziliweza kupatikana kutoka kwa Sista Yule. Wanatoa amri isiyokiukwa. Mandhari ya utekelezaji ya utingo na abiria ni moja. Utingo amepewa jukumu la kudadisi abiria anayezusha fujo daladalani. Anashusha kila abiria anapofika stesheni yake mahususi. Abiria wamesawiriwa kama wahusika wanaotekeleza maazimio yao kwa pamoja. Kwa pamoja walimvua ng uo sista Yule. Mzee na vijana ni wahusika waliotajwa tu katika hadithi ya Sista Yule.Hawakupewa majukumu maalumu.

### 2.4.3 Wahusika wadogo katika hadithi ya "Dakika za Adhama"

Katika hadithi ya 'Dakika za Adhama' ya Ngugi wa Thiong'o, kuna wahusika wadogo kama vile; Nyaguthii, Meneja, Bwana mwenye lori na askari. Nyaguthii ni msichana wa makamo aliyefanya kazi pamoja na Beatrice. Amepewa jukumu la ukinzani katika hadithi ya 'Dakika za Adhama' kwa sababu alikuwa mjeuri, mwenye mikogo lakini wanaume walijibana kwake.

Ni mpenda anasa mwenye kiburi na dharau. Baada ya kukinaika na mwenye klabu anamrusha kwa Beatrice. Alidhaminiwa na wateja wake. Mzee wa lori alipotaka kulala alimpa bunda la noti ili amhifadhie kwenye kaunta. Nyaguthii anaishi maisha ya kutojali, ndio maana amechukua mwelekeo wa starehe wala sio kwa kupenda. Alilelewa katika maisha ya Kikristo lakini alighairi na kutorokea mjini na hakuwahi kurudi nyumbani. Nyaguthii amesaidia kumjenga mhusika mkuu Beatrice katika hadithi ya 'Dakika za Adhama". Kutokana na vitendo vyake vilivyomuudhi, Beatrice anaishia kutenda aliyoyatenda ambayo hayakuwa makusudio yake.

Bwana mwenye lori ni mfanyibiashara anayependa kujistarehesha na wanawake vilabuni. Ni mhusika mwenye dharau na jasiri. Beatrice alipoiba pesa zake na kutoroka aliwachukua askari ili kumsaka. Meneja na askari hawajajengwa sana katika hadithi. Wametajwa tu ili kukamilisha kadhia.

### 2.4.4 Wahusika wadogo katika hadithi ya "Shimo la Maisha"

Wahusika wadogo katika hadithi ya 'Shimo la Maisha' na Raya Timmamy ni kama vile; Dadake Hamisi, baba mdogo, mkuu wa kitivo, mkuu wa chuo, mwenye kiti na majirani. Dadake Hamisi ni msichana aliyemlea Hamisi baada ya kuachwa na baba yao mdogo.

Alifanya kazi kwa bidii ili aweze kujikimu yeye na nduguye. Ni mwenye tumaini na nyota iliyong'aa maishani.

Naye baba mdogo ni mhusika aliyewalea Hamisi na dadake baada ya kifo cha wazazi wao licha ya kuwa na mapato madogo. Alimuelimisha Hamisi na dadake hadi kidato cha nne. Alijaa upendo kwa mayatima. Mkuu wa kitivo, mkuu wa chuo na mwenyekiti ni wahusika waliopewa jukumu la kusimamia wanafunzi wa chuo kikuu. Baada ya Hamisi kuandika barua mara tatu, walimpa mwaliko mbele ya kikao ili ajitetee.

### 2.4.5 Wahusika wadogo katika hadithi ya "Sami''

Katika hadithi ya 'Sami' iliyoandikwa na Mwenda Mbatia, wahusika wadogo ni kama vile; Mama Sami, Baba Sami, muuguzi, daktari Kogi, wakazi, meya, mkuu wa wilaya, jirani na mpenzi. Baba Sami na mama Sami ndio wanaoshughulikia matibabu ya Sami. Ni wenye siri na hawakubali ushauri wa daktari kuhusu ugonjwa wa mwanao Sami. Baba Sami anaposhauriwa na jirani amdadisi Sami kuhusu uhusiano wake na wasichana anaitikia kwa maana anahofia Sami asiwe hanithi.

Daktari na muuguzi wamepewa jukumu la kumtibu Sami na kumpa ushauri babake juu ya ugonjwa wake. Muuguzi ni mwenye matusi asiye na huruma. Kogi ni rafikiye Sami aliyeachiwa uongozi wa WAMA baada ya Sami kuugua na kushindwa kutekeleza wajibu wake. Hatokezi sana katika Hadithi hii.

Meya na mkuu wa wilaya walimsaidia Sami katika kuimarisha kikundi cha vijana wa majengo. Meya aliwapa vijana pesa za kununulia sare, viatu na mipira. Naye mkuu wa wilaya aliwahimiza kuanzisha chama.

### 2.4.6 Wahusika wadogo katika hadithi ya 'Namchukia Babangu'

Wahusika wadogo katika Hadithi ya 'Namchukia Babangu' ni; Mafutu, Mzee M'mali, Mama Bahati, Mfuata Mmali, Rahma, Kichomi na Mosi. Mzee Mkata M'mali ni tajiri mkubwa. Babake Mafutu, Rahma, Kichomi, Mosi, Mtoro na wengine. Kutokana na ufidhuli wake, mwanawe Mafutu alijitia kitanzi na Mtoro kutorokea mjini baada ya kumwibia babake pesa.

Mafutu M'mali ni mwenye hasira nyingi. Baada ya babake kukosa kumnunulia mkweche, aliamua kujiua. Ni mweledi wa masomo. Alipasi vizuri kwenye mtihani na kualikwa katika shule ya kitaifa. Kichomi ni dadake Mtoro M'mali aliyetoroshwa na nduguye na kuishia mjini. Amepewa jukumu la kulipiza kisasi dhidi ya babake. Yeye ndiye aliyekuwa chanzo cha ugonjwa ulioimaliza familia ya mzee Mkata M'mali.

Mosi ni mvulana wa mke wa pili wa mzee M'mali. Amepewa jukumu la kusambaza Ugonjwa lisilosikia dawa aliloambukizwa na Kichomi. Mfuata M'mali ni mkewe mzee Mkata M'mali aliyeolewa baada ya kifo cha mamake Mtoro. Rahma ni rafiki mkubwa wa Kichomi dadake Mtoro aliyefichua ukweli kuhusu janga lililotuliza jamii ya mzee Mkata M'mali kwa Mtoro M'mali. Bahati amesawiriwa kama mhusika aliye na bahati. Ni dadake mdogo Mtoro. .Ana ubinafsi wa hali ya juu. Baada ya kwenda ng'ambo aliwasahau nduguze na wala hakuwajali tena.kwa hivyo kwa ujumla wahusika hawa wamepewa nafasi finyu katika hadidhi hii.

### 2.4.7 Wahusika wadogo katika hadithi ya 'Fimbo ya Maradhi'

Wahusika wadogo katika Hadithi ya 'Fimbo ya Maradhi' ya Sam Ng'ang'a ni kama vile; Nyokabi, Thuo, Mzee Mponyaji, Njooki, Njeeri, Muthoni na Kihara. Thuo ni babake Ndugire

na mume wa Njooki, Njeeri na Muthoni. Ni mzee mwenye hekima. Ndugire alipoenda kwake kutaka ushauri alitumia hekima yake ili kumsaidia mwanawe aweze kumakinika. Ni mwenye amri isiyokiukwa. Kwa mfano aliamrisha kelele ikome nyumbani kwa Ndugire na kila mmoja akamtii. Ni kiongozi wa familia yake. Ni mdadisi wa mambo. Alitumia hekima yake kujua msimamo wa Njooki kumhusu mkazamwana Nyokabi.

Mzee Mponyaji (Mugo) ni mganga mwenye hekima ya hali ya juu na mwenye sarakasi na uigizaji wa hali ya juu. Nyokabi ni mkewe Ndugire na mamake Kihara. Anatuhumiwa kuwa mwovu na mama mkwe licha ya kuwa ni mwanamke mtulivu na msema kweli. Njooki, Njeeri na Muthoni wanshirikiana katika kutekeleza majukumu mengi. Ni wachochezi dhidi ya Nyokabi. Ni watiifu kwa sababu Thuo anapotoa amri wanatii bila maswali.

### 2.4.8 Wahusika wadogo katika hadithi ya 'Achekaye Mwisho'

Wahusika wadogo katika hadithi ya 'Achekaye Mwisho' ya Iribemwangi ni; Dennis Kitsakitsa, Boi, Sista Taziana na wakili. Dennis Kitsakitsa ni kijana mpole na mwenye roho ya utu. Ni mkaguzi wa mizigo pale uwanja wa ndege wa Wilson. Ni mwenye uvumilivu kwa mke wake. Ana roho ya huruma ya kutaka kuwafadhili wengine.wakati sista alipofutwa kazi alimfungulia hospitali ili apate mahali pa badala pa kujikimu na kujishughulisha.

Boi naye ni kijana wa umri mdogo aliyemuoa Binta baada ya talaka ya Dennis Kitsakitsa. Ni mwanasiasa aliyekuwa mlevi wa kupindukia. Wakili ametajwa tu katika hadithi.hakupewa nafasi yenye uzito. Kwa hiyo wahusika hawa wote wamepewa nafasi za kijuujuu tu.

## 2.4 Hitimisho

Katika sura hii tumeshughulikia wahusika katika hadithi nane miongoni mwa hadithi kumi na nne katika diwani *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* . kama ilivyobainika katika uchanganuzi wetu hadithi hizi zina wahusika wengi wadogo ambao wamepewa majukumu ambao wamepewa anuwai. Sifa walizonazo wahusika wakuu wa *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* ni zao la migogoro ya kisaikolojia au ya uhalisia wa maisha. Wahusika Sista na Yakubu wana migogoro ya kisaikolojia nao Hamisi na Sami wana migogoro inayotokana na kushindwa kwao kukabiliana na uhalisia wa maisha. Beatrice na Binta wana migogoro ya mapenzi ilhali Ndugire na Mtoro M'mali wana migogoro ya kijamii. Hii ni licha ya kuwa usawiri wao umebanwa na waandishi.

Kutokana na usawiri wao, tumeweza kubainisha kwamba wahusika wote wakuu ni wahusika bapa kwa sababu wamebuniwa kuzingatia matendo yanayooana na sifa walizopewa na kusawiriwa, na hawabadiliki sana. Ni sista Yule pekee ambaye anayembandilikabadilika lakini hata hivyo mabadiliko yake hayafiki ya wahusika wakuu. Waandishi wamefanya hivi kimakusudi ili kukidhi haja ya kusisitiza wazo kuu hasa juu ya wema au ubaya. Mhusika bapa hageuziki kwa sababu hakuviringwa na msanii na pia husafiri mawanda finyu. Hali hii ni tofauti na katika riwaya ambapo wahusika wanaweza kupitia viwango tofauti vya ukuaji kwa mfano katika riwaya ya Maisha kitendawili ya John Habwe, mhusika mkuu Farida amekuzwa tokea utotoni, akiwa mwanafunzi, mfanyikazi, mwajiri na hatimaye alipofunga ndoa.

Wahusika wasaidizi au wadogo wametumiwa na mwandishi ili kumsaidia msomaji kumwelewa vyema mhusika mkuu. Kupitia maingiliano yao na wahusika wakuu tunapata mwanga zaidi kuhusu hulka ya mhusika mkuu.

Katika uchunguzi wetu katika hadidhi nane tulizochanganua, tumebaini kuwa wahusika wote wadogo ni bapa kwa sababu hawakuzwi kikamilifu. Tumebaini pia kuwa idadi ya wahusika katika hadithi fupi ni ndogo ikilinganishwa na tanzu nyinginezo. Hii ni baadhi ya sifa za ubanifu katika hadithi fupi. Kwa mfano katika hadithi fupi ya '*Namchukia Babangu"* idadi ya wahusika ni kumi na tatu ilhali katika riwaya na tamthilia wahusika huwa zaidi ya idadi hii. Mfano mwafaka unapatikana katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* na John Habwe ambapo wahusika ni sabini. Idadi kubwa ya wahusika katika riwaya hutarajiwa kwa sababu riwaya huhusu mawanda mapana. Kwa hivyo kuwepo kwa wahusika wengi wenye majukumu anuwai hufanikisha malengo ya mwandishi. Wahusika katika riwaya na tamthilia husafiri mawanda marefu tofauti na ilivyo katika hadithi fupi jambo ambalo linasababisha tofauti hii ya idadi ya wahusika na ukuzaji wao.

Kwa hivyo wahusika wote wa hadithi fupi husawiri kwa njia ambayo inaafikiana na sifaya hadithi fupi nakuishia kubanwa ili kukidhi ukweli huu.

# SURA YA TATU

# MTINDO WA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA DIWANI YA *ALIDHANI KAPATA NA HADITHI NYINGINE*

## 3.0 Utangulizi

Uchunguzi wetu wa mtindo unahusisha kuangalia uteuzi wa msamiati, tamathali za usemi, mbinu za kibalagha, miundo ya sentensi, sura na upana wa aya zake, uakifishi wake. Nadharia hii inauangalia mtindo kama kitu chenye mchanganyiko uelezeao uhusiano uliopo kati ya mwandishi na kazi anayoifanya. Jinsi jambo linavyosemwa husaidia kuelezea na kufafanua maana ya kile kinachosemwa.

Katika sura hii tumejishughulisha na uchambuzi wa lugha katika kiwango cha maana. Tutaangazia jinsi mwandishi ametumia mbinu za lugha kwa ubanaji ili kuweza kuwasilisha maelezo hayo kupitia kwa wahusika. Tumejadili matumizi ya methali, semi, tamathali za semi: tashibihi, sitiari, tashihisi, tasfida, chuku, maswali ya balagha, majazi takriri, tanakali za sauti, kuchanganya ndimi na mdokezo. Pia tumeangalia mtindo wa sentensi fupi na sentensi ndefu. Mbinu hizi za lugha zinahusiana na maana mbalimbali kwa kutengemea muktadha zilipotumiwa. Katika uchanganuzi wa matumizi ya lugha tutaangazia jinsi ubanifu umedhihirika katika methali, semi, tamathali za usemi na mtindo wa sentensi.

## 3.1 Methali

Kuna maelezo mbalimbali yaliyotolewa kuhusu methali. Kwa ujumla fasili zote zinazotolewa huzingatia maana na matumizi ya methali husika. Mbatiah (2001), anatoa fasili kuwa methali ni kauli fupi iliyosheheni maana kwa ujumla, inayochukuliwa na jamii kuwa kiwakilishi cha ukweli na busara. Methali hubeba falsafa, mila, miiko, mbeko na desturi za jamii.Methali

huchukuliwa kama mkakati wa kisemaji ambao unaelezea sifa ya ubinafsi katika mazungumzo. Methali ni njia moja ya kuhalalisha usemi, uwe mzuri au mbaya.

Waandishi wametumia methali anuwai katika hadithi fupi zilizomo katika diwani ya *Alidhani kapata*. Katika hadithi ya Sista Yule, (uk 20) mwandishi anasema kuwa 'ikawa arobaini za Sista zimesalia muda mfupi tu.' Mwandishi ameitumia methali hii kuelezea tabia ya Sista ya wizi kuwa ilikuwa imefikia kikomo. Kwa kawaida methali hii huandikwa 'siku za mwizi ni arobaini"

Bakari aliweka mikakati mwafaka pamoja na sugusugu wa stesheni ya Somawani ndio siku ya arobaini ya Sista iweze kufika. Mtego wa kumnasa Sista ulimshika vizuri na kitendawili kikateguliwa bayana. Aidha katika hadithi ya 'Malimwengu' Methali, Aumwaye na nyoka hushtushwa na ung'ong'o Imetumiwa kuelezea zaidi tahadhari aliyokuwa nayo Lozi baada ya kuajiriwa kazi katika kiwanda cha kutengeneza blanketi mjini Maunguja. Alikuwa ameumwa na nyoka ya mimba na kutupwa na Bwana Mark Pacha. Akawa wakati huu anataadhari sana.

Mwandishi ametumia methali 'badala ya kufa kiu penye maji afadhali kufa kiu jangwani' (uk:113) katika hadithi ya 'Namchukia Babangu.' Methali hii imetumiwa kuelezea hali ambapo mtu anahitaji kitu fulani ambacho ni halali kwake kukipata lakini kimezuiliwa kimakusudi ikawa hawezi kukipata au kukitumia.

Mtoro M'mali pamoja na dada zake waliamua kutorokea mjini kwa sababu baba yao aliyekuwa tajiri mkuu aliwanyima haki zao kama watoto. Mtoro na nduguze waliishi maisha ya umaskini uliokithiri licha ya baba yao kuwa tajiri. Pia katika hadithi hii, methali 'Kila msiba huwa na mwenzake' (uk: 116) imetumika Methali hii inaelezea juu ya hali ambapo mtu hufikwa na matatizo yaliyofuatana moja baada ya lingine. mapacha wa Mzee M'mali

walipatwa na magonjwa wakawa mara Afrika Kusini, mara India, wapi! Uingereza, Marekani, wapi! Katika hali hii ya ugonjwa wa mapacha hali ya mama yao ikaanza kutia wasiwasi kisha ikawa baba, mama, kaka, dada wota hupitana angani huyu anaelekea Urusi huyo yuatoka huko. Ikawa shida kwa mzee Mkata M'mali zinavunja moyo sana.

Aidha katika hadithi ya "Namchukia babangu" Kichomi anasema kuwa siku moja nitakuja kufunza jizee hilo 'kilichomnyoa kanga manyoya' (uk: 117). Methali hii inarejelea hali kwamba alinuia kulipiza kisasi dhidi ya babake Mzee Mkata M'mali kwa vile alivyomchukia. Alipogundua kala tunda lenye dudu baya aliamua kulisambaza kwa mzee Mkata M'mali kupitia kwa nduguye Mosi. Katika hadithi ya 'Fimbo ya Maradhi' mwandishi ametumia methali 'Hauchi Hauchi! Unakucha! (uk:140). Inarejelea hali kwamba baada ya usiku mkuu lazima mwangaza uonekane kwa jambo lolote lile; mzee Thuo alijua kwamba, shida iliyokuwa imesababisha na kuzua utata mwingi katika boma yake ilikuwa karibu kuisha. Miale ya jua la tumaini ilikuwa imeanza kuangaza.

Mwandishi ametumia methali 'mambo ya mji huu yasianikiwe wageni' (uk:137) katika hadithi ya 'Fimbo ya maradhi.' Mzee Thuo anawaamuru wakeze kwamba yaliyokuwa yakitendeka katika boma yake yasije yakaelezewa watu wengine.Alitoa tahadhari kutokana na ugonjwa wa Ndugire uliosababisha kizaazaa katika boma ya Mzee Thuo kwa hivyo akatoa tahadhari hiyo Katika diwani ya *Alidhani kapata na Hadithi Nyingine,* methali zimetumika kudengua sifa ya ubinafsi na ubanifu na masaibu mengine yanayowapata wahusika. Methali hii zimetumika kibanifu na vile vile kuzitumia kumesaindia mwandishi kufafanua kazi yake kea maneno machache.

### 3.2 Semi

Wamitila (2003) anaeleza kuwa usemi ni neno lenye upana ambalo hutumiwa kuelezea matamko fulani yanayoelezea ukweli fulani. Aidha, semi ni kauli za maneno kadha yenye maana iliyofichwa. Waandishi mbalimbali katika diwani ya '*Alidhani Kapatana na Hadithi Nyingine*" wametumia semi nyingi katika hadithi tofautitofauti kuelezea hali fulani zinazowakumba wahusika. Kwa mfano, katika "Shimo la Maisha" mwandishi ametumia msemo 'chai ya mkandaa' (uk: 75) kuelezea chai aliyokuwa akiinywa Hamisi kila asubuhi. Chai ya mkandaa imetumiwa kudokeza zaidi juu ya umaskini walimoishi Hamisi na dadake. Pia katika hadithi hii mwandishi ametumia 'amekata kauli' (uk:81) usemi huu unaeleza juu ya uamuzi aliokuwa ameufanya Hamisi wa kuandika barua na kuomba apewe nafasi nyingine katika chuo kikuu baada ya kuanguka mtihani.

'Mungu si Athumani' ni semi iliyotumiwa katika 'Baiskeli '(uk: 1). Msemo huu una maana kuwa Mungu hana upendeleo na umetumika katika monolojia yake Yakubu juu ya tumaini alilokuwa nalo kwamba siku moja Mungu atamjalia kupata kijibaiskeli. Katika hadithi ya Dakika za Adhama usemi 'walipiga mtindi' (uk: 67) imetumiwa kuelezea kitendo walichokitenda Beatrice na Yule Kijana aliyemtorosha nyumbani na kumpeleka Nairobi huku akihadaiwa kutafuti wa kazi.

'Ulitumbukia nyongo' ni semi iliyotumiwa na mwandishi katika hadithi ya 'Namchukia Babangu'.Imetumika kutoa maelezo juu ya hatua ya mradi ulioanzishwa na utawala mpya kueleza kwamba mradi wenyewe haukufaulu. Mwandishi katika hadithi ya 'Fimbo ya Maradhi' ametumia semi 'akatoka shoti' (uk: 137). Msemo huu una maana ya kutoka kwa haraka na kuelekea mahali. Baada ya Mzee Thuo kusikia tafreni iliyokuwa katika nyumba ya mwanawe Ndungire alitoka mbio ili kuizima. Katika hadithi ya 'Sista Yule' semi 'kumpiga'

ngwara (uk: 16) imetumiwa kuelezea kitendo ambacho sista alifanyiwana Rasta Msimbo huu una maana ya kumbwaga mtu chini kabisa kwa nguvu. Rasta alimpokonya mwanamke begi akatimua mbio, Bakari akawa anafuata unyo unyo na kumbwaga chini.

Katika 'Malimwengu' Mapuza anatumia msemo 'amelala chali' (uk: 27) kuelezea hali aliyompata Lozi.Alikuwa amepatwa na kisunzi na kuanguka chini kifua juu. Pia katika hadithi hii semi 'amepigwa kalamu' (uk: 31) imetumiwa kuelezea kuachishwa kazi kwa Lozi baada ya mkurugezi Bwana Mark Pacha kungundua kuwa Lozi alikuwa mjamzito. Hawang'amui te wala be (uk:44) ni semi iliyotumiwa katika hadithi ya 'Bingwa kama mimi' Semi hii imetumiwa na mwandishi kuelezea hali ya wanafunzi wa chuo kikuu ambao hawaelewi chochote na wamezembea katika kazi. Kwa hivyo, kwa ujumla semi zimerahizisha nakurembesha maelezo huku zikiyabana kupunguzia mwandishi haja ya kueleza kwa marefu.

### 3.3 Tamathali za usemi

Kwa mujibu wa Mbatiah (2001) tamathali za usemi ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha katika viwango vya maana na mpangilio wa maneno ili kuleta maana mpya au msisitizo.

Naye Wamitila (2003) anasema kuwa Tamathali za usemi ni fungu la maneno au hata neno ambalo limegeuzwa maana yake ya kiurejelezi au asilia na kuwa na maana nyingine. Tamathali za usemi zina malengo mkubwa katika kuifanya kazi ivutie, iwe na msisitizo na mnato mkubwa. Mifano ya tamathali za usemi ni kama tashbihi, sitiari tashihisi, tasfida, chuku, maswali ya balagha n.k

### 3.3.1 Tashibihi

Tashbihi ni mbinu ya uhusiano na ulinganishi ambapo ukieleza kitu au sifa zake kwa kukilinganisha na kingine ili kuikuza sifa yake. Msokile (1992) anafafanua kuwa aina hii ya tamathali hutumia mlinganisho wa mambo ama vitu kwa kutumia viunganishi. 'kama', "mfano wa" "mithili ya","sawa na", na "mfano wa'' Mwandishi hutumia ulinganishi huu kusisitiza sifa fulani na pia kujenga picha ya aina fulani akilini.

Katika hadithi ya 'Dakika za Adhama' mwandishi anatueleza jinsi mwenye klabu alivyosisitiza wasichana waliohudumu katika klabu yake walale katika vyumba vya klabu.Hata hivyo, kusudi lake lilikuwa wasichana hao kutumia miili yao kama vivutio vya wanaume katika vyumba vya malazi vya starlight (uk: 61). Pia katika hadithi hii mwandishi anaeleza jinsi lori lilivyoonekana katikati ya magari mengine."Kabla ya kuingia, aligeuka mara ya mwisho na kufurahi kuona kuwa lori lake lililoonekana mithili ya ndovu miongoni mwa sungura." Katika dondoo hili, mwandishi anatuchorea picha ya jinsi mwenye Lori alivyowabeza Wenzake kwa kutokuwa na lori kama lake.

Kwa upande mwingine katika hadithi ya 'Shimo la Maisha' mwandishi anaeleza matarajio waliyokuwa nayo dadake Hamisi baada ya masomo ya chuo kikuu kwamba shida ingewaondokea.Aliona kuwa kama nduguye angelikuwa daktari basi huo ungekuwa kama ufunguo wa kuwafungulia kwingine. Mwandishi ametusaidia kujenga taswira juu ya kudhoofika kwa afya ya 'dadake Hamisi baada ya kuuguza. Alianza kumumunyuka kama udongo (uk: 77). Katika hadithi ya 'Sami' kuna matumizi ya tashbihi inayotusaidia kuelewa jinsi sura yake Sami ilivyokuwa kabla ya kupatwa na ugonjwa. Ile ngozi yake nyeusi kama mpingo nyororo na iliyometameta ilikuwa imeparara (uk: 99) Matumizi ya kama katika dondoo hili inatoa msisitizo na maelezo zaidi juu ya sura ya sami.

Mwandishi ametumia Tashibihi kuelezea juu ya afya ya mama katika hadithi ya 'Namchukia Babangu.' Baada ya Mtoro M'mali kuwatorosha ndugu zake kutoka 'Jehanamu' mama yao alipigwa na jitimai kubwa. Ugonjwa haukusikia dawa wala dua na baada ya mwaka mmoja wa kukonda mithili ya_sindano, mama akajifia (uk:113). Kwa kutumia maneno 'mithili ya Mtoro' M'mali anatoa mwangaza zaidi juu ya sababu ya mamaye kujifia. Tashbihi pia imetumiwa katika hadithi ya 'Fimbo ya Maradhi.' Mwandishi anaeleza hali aliyokuwa Ndugire baada ya ugonjwa wa kutunga. Macho aliyoyatambua yaliyowekwa kutoona chochote. Ndugire alikuwa mfano wa zuzu (uk: 138). Matumizi ya maneno 'mfano wa' ni ya kutilia mkazo wa hali ya Ndugire katika ugonjwa wake. Maneno haya yanazua maana zaidi kuliko kama hayangetumiwa.

Katika hadithi ya 'Sista Yule' kuna tashbihi inayotusaidia kuelewa tabia ya Sista ya kujitapa. Maneno aliyoyaelenzea utingo ni dhihirisho la haya. "Nyoo, mtusheheneze sawa na mifuko ya vitunguu. Sista alisema akijitengeneza mtandio wake kichwani. Matumizi haya ya tashbihi yanaeleza wazi kutoridhika kwa Sista Yule kwa jinsi wahaduma walivyosababisha msongamano katika magari ya umma. Kila mojawapo wa mifano hii umefupisha maelezo ya matukuo au hali zilizolengwa

### 3.3.2 Sitiari

Ni tamathali inayotumia viunganishi ambapo vitu viwili vilivyo tofauti kitabia na kimaumbile vinahusianishwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja. Mbatiah (2001) anaeleza kuwa sitiari huleta udhahiri na msisitizo katika maelezo. Sitiari hukuza sifa ya ulinganishi kwa kusema kitu fulani ni kingine. Tamathali hii ni muhimu katika kujenga taswira.

Katika hadithi ya 'Baiskeli' tunakutana na askari mfupi anayemkejeli Yakubu kuwa yeye ni nani na anafanya nini usiku barabarani wakati wa usiku. "Wewe ni mbwa? ...Eeh, Sema haraka. Wewe ni mbwa?" (uk: 30). Yakubu amelinganishwa na mbwa. Hivi ni kumaanisha kuwa mbwa ndiye mnyama aliye na ruhusa ya kutembea usiku barabarani bila kujali. Maelezo ya tabia ya wizi ya Sista katika hadithi ya 'Sista Yule yamejitokeza vyema katika mazungumzo ya abiria baada ya Sista kupatikana na simu za wizi.Sista amelinganishwa na chui aliyevalia ngozi ya kondoo. "Aisee kondoo kavalia ngozi ya chui!" "Ni chui kavalia ngozi ya kondoo" mwingine alimsahihisha (uk: 23). Matumizi ya maneno "Ni chui" yanaleta udhahiri na msisitizo juu ya tabia ya kinafiki Sista.

Maneno ya kuudhi ya muuguzi kwake Sami hospitalini katika hadithi ya 'Sami' ni maelezo ya tabia ya kubugudhi ya muuguzi. "Wewe ni tunda la mauti ambalo limeiva. Unajisumbua nini kuja hospitalini?" (uk:100). Mwandishi anapotumia maneno "wewe ni tunda la mauti" anazua ujengaji wa taswira juu ya hali ya samia na kudhihirisha tabia yake mbovu.

### 3.3.3 Tashihisi

Wales (2001) anafasili tashhisi kuwa ni tamathali ya usemi ambapo kitu kisicho na uhai, kisicho binadamu au chenye sifa za kidhahania kinapewa sifa za binadamu. Hivyo tashhisi ni tamathali ya usemi ambapo kitu kisichokuwa na uhai kinaelezwa au kuzungumziwa kama kwamba ni binadamu.Katika hadithi fupi ya "Baiskeli" tunaelezwa vile hali na wakati ulivyoenda mbio dhidi ya askari wa polisi "mfupi" na mrefu.' Mwandishi anatueleza kuwa. "...Pili wakati uliwakimbiza vibaya (uk: 7)". Wakati umepewa sifa ya kiumbe aliye hai na kuelezwa kuwa una uwezo wa kukimbia. Tunafahamu kuwa viumbe walio na miguu ndio wana uwezo wa kukimbia.

Kwingineno katika hadithi ya "Sista Yule" tunaelezwa maneno ya dhihaka ya abiria mmoja pale daladalani kuelekea Sanawari. "Twende! Kwani simu ni mtoto? Si ana mwanawe?" mwingine alidakia (uk:11). Simu imepewa sifa ya mtoto kwamba ni maarufu na ya maana kama mtoto. Aidha katika hadithi ya "Malimwengu" tunaelezwa juu ya hamu ya chakula (njaa) aliyokuwa nayo Lozi baada ya kupitia katika mateso baada ya wazazi wake kuaga. Kwa namna alivyoutazama mkunazi ungelidhani alikuwa anauambia: "Wewe ndiwe tumaini langu kwa nini usiniokoe?" Mkunazi umepewa sifa ya kuokoa maisha kana kwamba una mikono ya kushika na kumtoa mtu taabani.

Hadithi ya "Barua kwa Shangazi" inatoa maelezo ya mwandishi juu ya hali aliyokuwa nayo Shangazi kati yake na mumewe. "Baada ya chakula cha jioni nilijibwaga kitandani na usingizi ukaniiba mara moja" (uk: 42). Usingizi umepewa sifa ya kuiba kana kwamba unachukua bila ruhusa.

Katika "Dakika za Adhama" maelezo ya mwandishi kuhusu maumbile na tabia ya vilima vya Tumutumu yanazua hisia fulani.Ngoma na mapenzi yaliyoshuhudiwa na mbalamwezi huku vilima vya Tumutumu vikiinuka kugusa mawingu.Vilima vimepewa sifa ya kuinuka kana kwamba vina miguu ya kusimama.

Katika hadithi ya 'Shimo la Maisha" tunaelezwa namna Hamisi alivyohisi na hali ya mahali alimoishi. Aliishi mashimoni kule Kibera katika vyumba vidogo vidogo vya udongo tunaelezwa. Kwenyewe kumeitwa mashimoni kukaitika kwani vyumba hivyo vyote huonekana sawa kwa namna vilivyojengwa kwa matope. Mashimoni ni mahali ambapo pamepewa sifa ya mwanadamu. Tunaelezwa vizuri kwamba kiumbe aliye na uwezo wa kuitwa akaitika ni mwanadamu.

Hadithi ya 'Sami' inatoa maelezo ya jinsi umaskini ulivyokidhiri katika boma la Baba Sami, Vile kazi aliyoifanya haingeweza kukidhi mahitaji ya nyumba yake. "Hii ilikuwa kazi ya kijungu jiko tu. Haingeutikisa mlingoti imara wa chuma uliosimamia familia hii ukipeperushwa bendera ya umaskini" (uk. 100). Kazi ya babake Sami imepewa sifa ya uhai ya kutikisa mlingoti. Katika hadithi ya 'Namchukia Babangu' masimulizi ya Mtoro M'mali yanaeleza jinsi Mzee Mkata M'mali alivyowalea wanawe kiimla "Vipi nisiudhike nionapo dada zangu wawili walivyoteswa na dunia inayowakata mbele na nyuma mithili ya msumeno?" (uk: 110). Tunafahamu kwamba msumeno huwezo kukata huwa na makali. Dunia imepewa sifa ya kukata hali tunajuahaina meno.

Mazungumzo baina ya Ndugire na babake Thuo yanaangazia msimamo wa Thuo kumhusu mkazamwana Nyokabi kwamba hatafukuzwa kutoka nyumbani mwa Thuo. "Singetaka nikiwa hapa iwe mji wangu unanyoshewa kidole kama mji uliomfukuza mtoto wa watu kwa sababu ya uvumi." (uk:136). Kitendo cha kufukuza hutendwa na kiumbe aliye na uwezo wa kukimbia. Mji umepewa sifa ya kufukuza kana kwamba una miguu. Tashihisi hizi zote zimeeleza mambo anuwani kwa njia ya kimuhtari.

### 3.3.4: Tasifida

Wamitila (2003) anafafanua tasifida kuwa ni matumizi ya maneno ya kupunguza ukali. Badala ya mhusika kutumia lugha inayoudhi au ya matusi, anatumia lugha inayoficha makali hayo. Aghalabu tasifida hutumiwa baina ya watu ambao hawana budi kuwakikisha heshima katika mazungumzo yao.

Tasfida imetumika katika hadithi ya 'Baiskeli'. Tunaelezwa kwamba baada ya msako wa usiku huo mama mwenye mimba na Yakubu walitiwa ndani. Anaeleza kwa kukosa pesa za kutoa rushwa, Yakubu akalazwa 'ndani kwa mara ya kwanza maishani mwake (uk: 4) Mrefu alimuomba mwezake tena wamwachilie 'huyu mzee na Yule mwanamke mja mzito' (uk: 5). Maneno ya ndani inamaanisha seli wanakotiwa washukiwa kabla ya kufikishwa kortini. Matumizi mjamzito yanapunguza ukali ambao ungesababishwa na neno mimba. Katika hadithi ya 'Sista yule' tunaelezwa jinsi mama mtoto alivyopoteza simu mle daladalani. Abiria walizungumza mengi. Akaambiwa aweke pesa kidogo kidogo ili anunue lingine. Tunasoma: Hawa sawa na kozi aliyekuwa kifaranga! Tunduiza hela ununue nyingine - hesabu hasara (uk: 1). Neno tunduiza linapunguza uzito kuliko kutumia neno weka akiba polepole.

Hadithi ya 'Malimwengu' ina matumizi ya tasfida. Lozi alipoanguka akawa hajijui hajitambui, bibi alisongea karibu na kumdadisi. Bibi aligundua eeh! Lozi yuko taabani: Alikuwa yuko njiani akielekea kwa muumba wake. (uk: 28). Matumizi ya maneno 'njiani akielekea kwa muumba wake' yanapunguza ukali badala ya kufariki. Tasifida imetumika katika hadithi ya 'Barua kwa Shangazi' tunaelezewa juu ya hisia alizokuwa nazo Raeli wakati alikuwa akimwandikia barua Shangazi. Huenda nimekuchosha kwa barua ndefu. Lakini ikiwa singekuandikia, ningeishia kwa daktari wa akili. (uk: 40). Ningeishia kwa daktari wa akili ni maneno yanayotumika ili kupunguza uzito wa kurukwa na akili.

Katika hadithi ya 'Shimo la Maisha' mwandishi anaelezea jinsi alivyosumbuka naHamisi katika maisha ya umaskini .Alifanya kazi ambayo malipo yake hayangekidhi mahitaji yake. Anaeleza; alifikiria jinsi angekosa zile pesa za kijungu jiko alizokuja kutegemea sana. Pesa za kijungu jiko ni maneno yanayopunguza uzito wa kidogo au zisizotosheleza mahitaji.

### 3.3.5 Chuku

Hii ni mbinu ambayo hutumiwa kupunguza sifa ya kitu au mtu kwa lengo la kudunisha. Mbatiah (2001) anasema kuwa chuku ni tamathali ya usemi inayotumia lugha ya kutilia chumvi aghalabu kwa madhumuni ya kusisitiza jambo au kurejelea hali hukuzwa kupita kiasi. Nia ya kuitumia chuku ni kupunguza sifa fulani litokeze kwa uwazi zaidi ili kuikuza sifa hiyo. Katika hadithi ya Achekaye Mwisho tunaelezwa jinsi wapinzani wake Boi walivyoongeza chumvi katika usemi wao wakati wa siasa walieneza uvumi ili kumdunisha Boi.

Tunasoma;

Uvumi zaidi ulienezwa kuwa Boi alikuwa na usahibu wa kimapenzi na Binta hata kabla ya binta kupata talaka na kufungaa ndoa naye. Wengine walidai kwamba aliyekuwa mumewe Binta alishakuwa mwenda wazimu na alionekana akiokota taka mjini (uk 165) Katika dondoo hili mwandishi anapiga chuku Maneno ya wapinzani wa Boi waliyoyaeneza madai haya ili kumpiga vita. Mwandishi anatueleza juu ya hali ya Yakubu jinsi alivyoonekana kisura: Kijana wa miaka thelathini na mitatu alionekana kama mzee wa miaka hamsini (uk: 2) Sababu ya maelezo haya ni kusisitiza juu ya umaskini na taabu aliyokuwa nayo Yakubu.

Mwandishi amepiga chuku anapotoa maelezo juu ya jinsi mama mtoto alivyoshuka kutoka daladalani. Utingo anauliza; "Aisee dada", utingo alimfoka "ndio ikuchukue mwaka kushuka?" (uk: 21). Maneno 'ikuchukue mwaka kushuka?' yanapiga chuku kujikokota kwa mama mtoto. Pamoja na kufafanua hali na matukiozimefunika kuchora picha kwa maneno machache.

### 3.3.6 Maswali ya balagha

Hii ni tamathali ya kuuliza maswali ambayo hayahitaji majibu. Aghalabu maswali hayo hayahitaji majibu kwa sababu majibu yake yako wazi kwa msikilizaji au msomaji. Ni mbinu moja ya kusisitiza usemi, kumfikirisha msomaji na kumshawishi kuhusu jambo. Waandishi wa hadithi mbalimbali katika diwani ya *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* wametumia maswali ya aina hii. Kwa mfano, katika hadithi ya 'Barua kwa Shangazi' mwandishi anaeleza mateso aliyopitia Raeli baada ya kifo cha mumewe anasema. Nilistaajabu ya Musa; kumbe ya Firauni yalikuwa nyuma? (uk:39)

Katika hadithi ya 'Sami' mwandishi anaeleza maneno ya ukali aliyotumia muuguzi pale hospitalini akimwambia Sami kwa kumwambia; "Wewe ni tunda la mauti ambalo limeiva. Unajisumbua nini kuja hospitalini? Kuharibu dawa bure (uk: 100). Maswali ya balagha yametumiwa katika hadithi ya 'Nachukia Babangu'. Maneno ya Mtoro M'mali kumhusu babake ni bayana kupitia maswali ya balagha: Anasema 'Na vipi nisikereke nijitazamapo nilivyo? Vipi nisiudhike nionapo dada zangu wawili walivyoteswa na dunia inayowakata mbele na nyuma mithili ya msumeno? Nisiumwe nimkumbukapo marehemu kaka Mafutu?'(uk: 110). Katika hadithi ya 'Naye huyo, Mme Mwenzangu?' Mwandishi anatumia maswali ya balagha kuelezea wasiwasi aliokuwa nayo mumewe Shamsa. Baada ya kungojea kwa muda alianza kujisemea.Vipi leo? Mbona haonekani? Si miye mwenyewe nimemwona pale dukani lake la urembo? (uk: 149)

Maswali ya balagha yametumiwa katika hadithi ya 'Achekaye Mwisho.' Baada ya Dennis kufunga pingu za maisha na Binta, mambo yaligeuka na kuwa kinyume na matarajio yao. Dennis anauliza; Ndoa! Unyumba! Hii ndiyo maana yake? Mungu wangu! Kwa nini nikajiingiza kwenye uendawazimu huu? (uk:159)

### 3.3.7 Majazi

Hii ni mbinu ya kuwapa wahusika majina ambayo yanaakisi vitendo na tabia zao. Jina la mhusika linakuwa kidokezo kuhusu uhusika wake. Majazi huhusisha pia majina ya mahali. Mbinu hii humsaidia msomaji kufahamu sifa na tabia ya mhusika kwa urahisi sana. Aidha, inaweza kuweka wazi mtazamo wa mwandishi kuhusu wahusika fulani na hata kutoa mwelekeo wa hadithi nzima.

Katika hadithi ya 'Baiskeli' tunampata mhusika Yakubu Bahati ambaye anafanya kazi ya sulubu. Yakubu Bahati amepewa jina hilo ambalo linaafiki tabia yake ya kuwa na bahati. Yakubu amesawiriwa na mwandishi kama mtu anayemwamini Mungu. Alitamani siku moja ajaliwe kupata baiskeli. Mwishowe Yakubu anabahatika kupata baiskeli pasi kuinunua. Mfupi na mrefu ni majina ambayo ni ya kimajazi. Mfupi alikuwa mfupi kwa kimo na pia mrefu alikuwa mrefu kama jina lake linavyoashiria.

Jina la'Bibi' katika hadithi ya 'Malimwengu' linaakisi tabia ya kawaida ya Bibi. Bibi alikuwa bibiye Lozi aliyemlea baada ya wazazi wake kuaga dunia. Anamtetea dhidi ya mateso kutoka kwa shangazi. Aidha jina la 'Lozi' ni la kimajazi kwa kuwa yeye ni mbegu kutoka kwa wazazi wake yaani nimzawa. Katika hadithi ya 'Shimo la Maisha' jina la Mashimoni ni jina la kimajazi. Mashimoni ni mahali walimoishi Hamisi na dadake. Nyumba za mahali pale zilijengwa kwa matope. Hivyo mtu alipoingia ndani ilikuwa ni sawa na anayeingia shimoni kwani kulikuwa na giza.

Hadithi ya 'Namchukia Babangu' ina majina ya kimajazi; Mtoro M'mali, Mkata M'mali' Mfuata M'mali, Mafutu Kichomi, Bahati na Mosi yote ni majina ya kimajazi. Jina 'Mtoro'

linamaanisha mtu anayetoroka kwao. Mtoro M'mali alitoroka nyumbani kwao na kuelekea mjini alikoishi maisha ya kurandaranda ovyo. Alitoroka mali ya mzee M'mali ambayo haikumsaidia. Mkata ina maana ya mtu asiyekuwa na chochote, yaani fukara. Licha ya Mkata M'mali kuwa na mali nyingi, aliishi maisha ya ukata yeye pamoja na jamii yake. Mfuata ni jina linalomaanisha kufuata 'Mfuata ni mwanamke aliyeolewa na mzee M'mali baada ya kifo cha mkewe. Mfuata alikuwa ameitembea dunia, kapewa talaka tatu na kuwa na watoto watano. Hivyo yeye alimfuata Mzee M'mali ili aweze kukidhi mahitaji yake.

Jina la 'Mafutu' ni la kimajazi. Linamaanisha hali impatayo mtu anapokasirika au kughadhabika. Mafutu alikuwa yu radhi kufanya lolote pasi kuliweka kwenye mizani mara ya pili. Baada ya babake Mzee M'mali kukataa kumnunulia mkweche alijinyonga. Kichomi ni dadake Mtoro M'mali ndiye aliyemuambukiza Mosi gonjwa baya. Kutoka kwa Mosi lile dudu baya lilizagaa katika mji wa Mzee mkata M'mali na Bi. Mfuata M'mali kama moto wa nyika wakati wa kiangazi. Hivyo Kichomi akauchoma msitu mzima wa boma ya mzee M'mali. Bahati naye alibahatika akachukuliwa na Wazungu fulani, akafunzwa vyema na baadaye wakaenda naye ng'ambo. Nduguye alimsaka na wala hakupatikana. Mosi ni jina linalomaanisha awali au lililotangulia. Mosi ndiye aliyekuwa mtoto wa kwanza wa Bi. Mfuata M'mali.

Katika hadithi ya 'Fimbo ya Maradhi' jina la mzee mponyaji limetumika kimajazi. Alipomshauri Ndugire kuepuka kizaazaa alichokuwa nacho baina yake na mkewe Nyokabi. Ndiye aliyeleta uponyaji wa kimwili na kisaikolojia katika boma ya mzee Thuo.

Maneno ya kimajazi yametumika kunasa taswira na maelekeo ya wahusika hawa na .....haya ya kuwaeleza sana.

### 3.3.8 Tanakali za sauti

Hii ni mbinu ya uigaji wa sauti fulani. Msingi mkuu wa matumizi ya mbinu hii ni kuhakikisha kuwa hali fulani imeelezwa kwa njia kamilifu. Maneno yanayotumiwa huonyesha jinsi sauti fulani inayosikika. Mbinu hii imetumiwa ili kutueleza namna gari zito lilivyonguruma katika hadithi ya Naye huyo M'me Mwenzangu? Inalia Vruuum! Sauti ya gari zito imesikika (uk:149). Aidha katika hadithi ya 'Achekaye Mwisho' tunaelezwa jinsi muda ulivyosonga na mlio wa simu ukasikika. Bado dakika nne, ...tatu ....mbili ....moja mara, "krrrr, krrrrr" simu ikaita (Uk: 158).

Hadithi ya 'Dakika za Adhama' kuna matumizi ya tanakali za sauti inayoeleza juu ya sauti aliyoitoa Beatrice baada ya kuhisi kuwa anadharauliwa na mpenziwe. Alipofika hapo, Beatrice alianza kulia kwa kwikwi (uk: 68). Katika hadithi ya 'Malimwengu' mwandishi anatueleza jinsi Lozi alivyoanguka baada ya kuhisi kizunguzungu na akaona kana kwamba dunia inazunguka akapoteza mwelekeo na kuanguka pu! Kama gunia shinda (uk:27). Hadithi ya 'Naye huyo, Mme Mwenzangu' moyo ulivyomdunda Shamsa baada ya mpenziwe Badi kuingia nyumbani na kumuomba atoke. Anaeleza: "Tutoke? Twende wapi?" Shamsa sasa moyo ni du...du...du! (uk: 151). Katika hadithi ya 'Malimwengu' mwandishi anaeleza jinsi tumbo lake Lozi lilivyonguruma na michango ya milio. Anaeleza: "Lozi ulisikika kwa mara nyingine na kwa nguvu zaidi, Churuuru! Churuuru! Churuuru!" (uk: 28). Matumizi ya tanakali ya sauti zinapatia hadithi hizi uhalisia kwa sababu mambo yanahisika kuwa halisi na kuondoa haja ya maelezo marefu.

### 3.3.9. Mdokezo

Hii ni mbinu ambapo mwandishi anamkatiza usemi fulani na kumwachia msomaji kuumaliza mdokezo unaweza kutumiwa kuashiria maarifa fulani. Mdokezo pia unaweza kusababishwa kwa sababu ya tasifida. Mfano katika hadithi ya 'Baiskeli' Yakubu anapotaka kujieleza mbele ya askari polisi anasema:

"La, la, mim..." alianza kunena Yakubu lakini Yule afisa mrefu akamkatiza (uk: 3). Aidha katika hadithi ya 'Malimwengu', Furaha anapomliwaza Lozi baada ya kupigwa kalamu na kufurushwa na Bwana Mark Pacha; "Huu si wakati wa kulia, chukua virago vyako hurudi nyumbani. Hii jiji..." (uk:33)

Katika dondoo hili Furaha anamueleza Lozi kuwa jijini kuna mengi ya kustajaabisha na hivyo ajipe moyo.

Katika hadithi ya 'Namchukia Babangu' mwandishi anaeleza jinsi Mtoro M'mali anavyomwazia babake Mzee Mkata M'mali. Anasema "Mzee M'mali hajui kama sote tu hai au tu wafu. Na hajali. Ama labda anajali kwa sasa..." (uk:115).

Hadithi ya 'Fimbo ya Maradhi' ina mdokezo. Babake Ndugire anamueleza mwanawe kuwa haitakuwa vyema kumfukuza Nyokabi kutoka pale nyumbani. Amesema 'Mwanangu si busara kumrudisha Nyokabi kabla ya kudhibitisha madai anayohusishwa nayo..." (uk:136).mdokezo ulivyotumuka katika diwani hii unafupishaa maelezo na kumpatia mwandishi nafasi ya kukuza kisa kimuhtasari.

### 3.3.10 Kuchanganya ndimi

Hii ni mbinu ambapo mwandishi anatumia lugha mbili au zaidi kwa kuchanganya. Sababu kuu ni kuonyesha tofauti za wahusika kwa matumizi ya lugha. Katika hadithi ya 'Sista Yule'

kuna matumizi ya maneno kama vile '*t-shirt'* za lebo ya '*Fifty cent'*, *Samsung x660'*, '*Lollipop*' (uk: 18)

Hadithi ya 'Bingwa kama mimi' matumizi ya lugha mbili yadhihirika katika (uk: 53) na 54: 'Come in' 'Then get out of my office', 'I am busy', 'why?' (uk: 52)

Hadithi ya 'Dakika za Adhama' matumizi ya majina ya kiingereza yanadhihirika: Treetops, Jukebox, pia matumizi ya maneno ya Kikuyu, Huñyu wa mashambani' (uk: 70)

Katikia hadithi ya 'Sami' Daktari anapomshauri Baba Sami anatumia neno 'Absolutetly' (uk:100). Matamshi ya maneno "*Eureka, Eureka*" yametumiwa katika hadithi ya 'Namchukia Babangu.' Maneno *Eureka, Eureka* yanaashiria jambo la kustaajabisha (uk:112). Mafutu alimwendea babake Mzee Mkata M'mali kumwomba amnunulie baiskeli.

Katika hadithi ya 'Pendo la Siri'mbinu ya kuchanganya ndimi imetumiwa na mwandishi. (uk:124) Mwandishi ametumia maneno 'Taarab night', 'Audhubillahi', 'ya Rabbi'.

Hadithi ya 'Naye huyo M'me Mwenzangu 'kuna matumizi ya maneno kama vile; Hello! Hello (uk: 147), 'sweethearts' na 'darlings' (uk:148), 'Security sevices' (uk:149) 'uncle'. Katika hadithi ya 'Achekaye Mwisho' matumizi ya maneno kama vile: 'Well beauty comes at a cost', and have a nice, time,' Thank you'' '*business card'*, call any time '*boy friend'* (uk: 156). Matumizi ya maneno haya yanadhihirisha kuwa wahusika hawa wanaufahamu wa lugha mbili na wanaweza kuzitumia katika mawasiliano yao.

### 3.3.11 Takriri

Takriri ni urudiaji wa silabi, maneno, msitari au vifungu vinavyolingana katika kazi ya sanaa kama anavyosema Msokile (1992). Lengo kuu la mwandishi kurudiarudia maneno au vipengele hivyo ni kutilia mkazo jambo linaloelezwa. Kwa mfano katika. 'Malimwengu' mwandishi anasisitiza kitendo cha Shutu kumwita Mapuza, anaita; Mapuza! Mapuza! Mapuza... (uk: 27) Pana urudiaji wa Mapuza. Hii ni takriri ya maneno.

Katika Hadithi ya 'Alidhani kapata' pana matumizi ya takriri ya mwandishi anaeleza jinsi mtu anavyopaswa kujenga katika ulimwengu wa leo. Anasema:

'Ulimwengu wa leo ni kutoka, ukaona, ukalenga, ukafuma. Basi lakini 'Darling voltaire' lina ladha kutamka, kuandika,kujulisha kwa watu.' (uk: 85)

Katika dondoo hizi pana takriri ya "uka" ya kumrejelea mhusika Vicky. Takriri ya "ku" inarejelea kitenzi katika dondoo. Takriri ya Mofu inadhihirika.

Katika hadithi ya 'Namchukia Babangu' kuna takriri katika maelezo ya Mtoro kuhusu ukubwa wa nyumba zilizomilikiwa na babake. Tunaelezwa:''Ana viwanda na majumba makubwa makubwa ya kukodisha... (uk 111). Mwandishi pia anasisitiza unyenyekevu wa mafuto kwa babake kutokana na namna anavyofanya ombi lake la kununulia gari. Anamsihi: ''...japo iwe mkweche nitashukuru nitashukuru (uk 112).

Tabia ya mzee ya kufuja pesa inasisitwa ifuatavyo: 'Hakuhifadhi pesa tena mzee huyo, kutoa na kutoa... (uk 116). Katika dondoo hili kuna urudiaji wa neno kutoa kuleta maana ya kusisitiza hali ya kutoa

### 3.4 Sentensi fupi

Sentensi inaweza kuwa fupi ikiwa na maneno machache mradi tu mwandishi anaeleza wazo Lake Kikamilifu. Inaweza kuwa ya neno moja maneno mawili au matatu mradi ina kiima na kiarifu ndani yake.

Mohammed S.A (1995) anasema kuwa kazi muhimu ya sentensi fupi mara nyingi ni kujenga hisia ya uchangamfu, harakati woga, hofu au wasiwasi. Kwa ajili ya ufupi wa sentensi kunapatikana mapigo ya mizani mafupi mafupi.

Katika 'Baiskeli' tunaelezwa hali ya Yakubu Bahati ya kutembea miguu hadi kazini. Aliendelea kuchapa guu. Hakuwa na jingine. Dondoo hili linaonyesha harakati ya Yakubu ya kwenda kazini. Pia linadhihirisha shida zake. Kwingineko katika hadithi ya 'Sista Yule', harakati ya kumnasa mwizi wa begi zinadhihirisha matumizi ya sentensi fupi. Kamata! Piga rungu! Acheni! 'Msimpige! Tumfikisheni kituoni!. Sentensi hizi fupifupi zinatudhihirishia hisia na hofu walizokuwa nazo raia baada ya kumnasa mwizi wa begi. Katika 'Barua kwa Shangazi'maelezo ya Raeli kwa shangazi yake juu ya uhusiano wake na mashemeji. Anasema; Nimevurugana na mashemeji vibaya. Nimewalaani. Wamenilaani. Natamani amani. Nami siwaelewi. Utamanduni wao umenishinda. (uk:37). Sentensi hizi zinaangazia juu ya hisia na hofu zake Raeli kwa mashemeji wake. Hadithi ya 'Sami' Mwandishi anaazisha hadithi kwa matumizi ya sentensi fupi. Anaeleza; Mama Sami! Baba Sami alipaza sauti. Mimi natoka sasa. Safari ya wapi? (uk; 98)

Katika hadithi ya 'Namchukia Babangu' maelezo ya Mtoro M'mali kuhusu familia ya mzee M'mali yanasaindia kujenga taswira juu ya hali ilivyokuwa katika boma la Mzee Mkata M'mali "Lakini sio hao tu. Mzee mkata M'mali pia. Na watoto watano. Kisirani kipi hiki?

Uchawi uliokithiri" (uk:116) Ni dhairi kuwa sentensi fupi mara nyingi zina muhimu wa kujenga hisia za uchangamfu, harakati, woga, hofu wasiwasi au hata taharuki. Sentensi fupi ni kutambulisha muhimu cha hadithi fupi kwa uwa mwandishi hana fursa ya kufafanua mambo kwa marefu na mapana.

### 3.5 Sentensi ndefu

Unaposoma kazi fulani unaweza kukumbana na sentensi ambazo zimetumia maneno ya idadi kubwa tofauti na sentensi fupi ambayo inaweza kuwa ya neno moja. Urefu wa sentensi unadhihirika kwa matumizi ya viunganishi kama 'na' 'wala' 'lakini' 'au' na 'tena' ambayo huunganisha maneno na sentensi za aina hii huitwa sentensi ambatani. Matumizi ya sentensi ndefu yanadhihirika katika hadithi ya 'Namchukia Babangu' mwandishi kupitia usimulizi wa Mtoro M'mali anaeleza chanzo cha dudu mbaya lililozagaa katika mji wa mzee mkata M'mali anaeleza:

"Naye Mzee Mkata aliwaendea mabinti wote hawakuwa wanawe halisi alijituliza na kwa kutumia mapesa yake akaweza kucheza ngoma goya nao (nani alisema kwamba simba mzee asile nyama au paka mzee asinywe maziwa? Alinungunika mara kwa mara" (uk:117).

Katika 'Achekaye mwisho' tunaelezwa jinsi Binta alivyomtegemea mumewe Dennis kwa matakwa yake yote.

"Dennis ndiye amlipie rent ya ofisi, alipe wafanyikazi, bill za simu, umeme na maji kila kitu na juu ya hayo ampe yeye pesa za kumkidhi mahitaji yake ya kila siku, na haya hayakuwa haba (uk: 159)"

Vile vile matumizi ya sentensi ndefu yanadhihirika katika hadithi ya 'Baiskeli,' mwandishi anaeleza juu ya maombi ya Yakubu anaeleza:

"Siku hiyo maombi yaliendelea nusura ifike saa moja, lakini Yakubu hangethubutu kutoka kwa kuwa hakuna jambo lililompa amani na utulivu duniani kama ushirika wa maombi, mahubiri na nyimbo kwa muumba wake" (uk: 3).

Hadithi ya 'Malimwegu' ina matumizi ya sentensi ndefu. Hii inadhihirika katika maelezo ya mwandishi juu ya ndoto yake Lozi ambalo alikutimia. Anaeleza:

"Lozi alikuwa na ndoto ya kusoma hadi kufika chuo kikuu. Lakini wazazi wake walipofariki na kuachwa mikononi mwa shangazi Mashaka, ndoto yake iliyeyuka kama barafu hasa wakati alipokatishwa masomo ya shule ya msingi na akawa kijakazi wa Shangazi Mashaka" (uk:30)

Sentensi ndefu ni ukiushi katika hadithi fupi. Aghalabu sentensi huwa fupi fupi. Kwa kawaida miktadha iliwalazimisha waandishi kutumia sentensi ndefu.

### 3.6 Hitimisho

Katika sura hii tumeangazia uchambuzi wa kimtindo. Tumeangazia matumizi ya methali na semi mbalimbali na kutoa mifano anuwai kutoka hadithi mbalimbali ili kuthibitisha hoja zetu. Aidha, tumeangazia namna tamathali za usemi zilivyotumiwa ili kutoa mnato wa kisanaa. Tamathali za usemi hudhihirisha ukomavu wa mwandishi. Pamoja na kupitisha ujumbe. Baadhi ya tamathali za usemi ambazo tumeangazia ni pamoja na tashbihi, sitiari, tashhisi, tasifida, chuku, maswali ya balagha, majazi, takriri, kuchanganya ndimi na mdokezo.

Pia tumeangazia sentensi ndefu na fupi.Tumegusia ufupi na urefu wa sentensi katika diwani ya Alidhani Kapata. Tumebainisha kuwa mwandishi amechanganya sentensi fupi fupi na sentensi ndefu ambazo zimedhihirishwa katika baadhi ya hadithi.

Uchanganuzi wetu umedhibitisha kuwa mbinu za matumizi ya lugha katika Hadithi fupi ni mahsusi. Tumegundua kuwa maneno yanatumiwa kwa mnato na ujumi mkubwa ili kuhakikisha kuwa ujumbe unafikishwa kwa wasomaji kwa ukamilifu na kusababisha athari inayodhamiriwa. Ni bayana kuwa pamoja na kuwakikisha ujumi istilahi na kauli tofauti zilizotumika zimedhihirisha ubanifu ambao ni sifa yakimsingi ya utanzu wa hadithi fupi,

# SURA YA NNE

# MATUMIZI YA DAYOLOJIA NA MONOLOJIA KATIKA DIWANI YA ALIDHANI KAPATA NA HADITHI NYINGINE

## 4.0 Utangulizi

Dayolojia na monolojia ni sifa za kimuundo kwa kuwa mwandishi anapotumia dayalojia na monolojia anaifanya kazi yake kuwa na sura tofauti. Dayolojia na monolojia pia zinaweza kutumika katika usawiri wa wahusika vile vile dayolojia aghalabu huyafanya maudhui kuelezeka kibayana.

Katika *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*, waandishi wametumia mbinu nyinginezo za matumizi ya lugha. Mbinu hizi mjarabu zimetumiwa ili kufanikisha kazi mbalimbali za kisanaa. Katika sehemu hii, tumeshughulikia dayalojia na monolojia.

Dayolojia na monolojia ni kati ya vipengele muhimu vya fani ambavyo pia vina nafasi kubwa katika drama. Tumechanganua vipengela hivi kwa kuangazia namna vinavyotumiwa kujenga na kukuza hadithi. Kimsingi, hivi ni vipengele vya fani ambavyo hutumiwa na mwandishi wa hadithi kuwasilisha ujumbe wake. Kwa hivyo dhamira na maudhui ya hadithi huwasilishwa na mwandishi kikamilifu kupitia kwa namna anavyokuza mazungumzo ya wahusika. Dayolojia na monolojia huhusu mazungumzo ya wahusika. Tofauti baina ya vipengele hivi ni kwamba dayolojia ni mazunguzo kati ya wahusika wawili au zaidi au majibizano baina ya wahusika wawili au zaidi ilhali monolojia ni maelezo ya mhusika mmoja bila kujibizana na mhusika mwingine. Matumizi ya dayolojia na monolojia yamedhihirisha ubanifu katika hadithi tulizoziteua katika sampuli yetu.

## 4.1 DAYOLOJIA

Kuna aina nyingi za dayolojia kama vile:

i) Dayolojia shawishi ambapo lengo la kila mhusika huwa ni kumshawishi mwenzake akubali jambo fulani.

ii) Dayolojia ulizi, ambapo msemaji hutaka kujua zaidi, kuhusu jambo Fulani.

iii) Dayolojia malumbano, ambapo wahusika hubishana au kujibizana n.k

Wamitila, (2008) akimnukuu Short (1980), alisema kuwa dayalojia ina miktadha mitatu mikuu; muktadha wa kimaumbile, ambao unarejelea mtagusano baina ya wahusika kwenye mandhari halisi kama vile hotelini, mahali pa hadhara, nyumbani, shuleni, njiani n.k. Muktadha wa aina hii hujenga nguzo muhimu za mazungumzo ya ana kwa ana baina ya wahusika. Pia, alizungumzia muktadha wa kibinafsi ambapo huonyesha mahusiano ya kibinafsi na kijamii baina ya wahusika katika mazungumzo. Uhusiano huo unaweza kuwa wa kijamaa (baina ya mtu na mkewe, mtoto na mzazi, baba na mjukuu n.k) wa kizazi n.k. Muktadha huu huathiri mada ya mazungumzo, sajili, msamati n.k.

Muktadha wa kimaarifa/ kiakili ni wa tatu aliojadili Wamtila (2008). Huu hurejelea maarifa waliyonayo wahusika katika mazungumzo. Maarifa waliyonayo wahusika yanaathiri mazungumzo yao. Miktadha hii ni muhimu kwa sababu itasaidia katika uchambuzi wa lugha na sifa za kiusemi. Mazungumzo ya wahusika ni muhimu sana katika ujenzi wa dhamira na maudhui ya hadithi fupi. Mwandishi anawezakuthmini, hasa kupitia mazungumzo ili kuhakikisha kwamba amewasilisha ujumbe anaotaka ipasavyo. Kwa hivyo itambidi kuchuja na kuteua mambo yale muhimu na mazito, kutosha kuupeperusha ujumbe wake.

Dayolojia katika hadithi fupi ni mbinu mojawapo ya zile ambazo hutumika na mwandishi kuwasilisha ujumbe. Jinsi msimulizi anavyotumia dayolojia ndivyo aonyeshavyo umahiri

wake katika uwasilishaji wa ujumbe. Dayolojia huonyesha uwezo wa mwandishi wa hadithi fupi, wa kuwasawiri wahusika wake, ili kuwasilisha ujumbe. Kwa namna fulan. Anapotumia dayolojia, mwandishi huweza kutofautisha wahusika wake. Kuna wale wahusika watakaoonyesha ujuzi wao katika kutumia lugha kama vile; matumizi ya lahaja, ujuzi wa lugha zaidi ya moja, lugha chapwa, utumiaji wa lugha chakavu, lugha ya kishairi n.k. Hivyo ni rahisi kumtenga mhusika na wengine kulingana na lugha wanayoitumia katika hadithi fupi inayoshughulikiwa.

Mazungumzo katika *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine* yametumiwa na mwandishi kama mbinu mojawapo ya kuwasilisha ujumbe. Zaidi ya hayo, mwandishi ametumia dhamira, kuonyesha maarifa waliyonayo wahusika na pia kuonyesha mandhari fulani wanamozungumzia. Mwandishi ametumia dayolojia- shawishi, ulizi, na majibizano ili kuwasilisha ujumbe wake.

### 4.1.1 Dayolojia shawishi katika diwani ya Alidhani Kapata' Hadithi Nyinginezo

Hii ni dayolojia ambapo mhusika mmoja hutumia maneno shawishi kwa mhusika mwingine ili jambo fulani lipate kutendeka na hata kutimia. Dayolojia shawishi imedhihirika katika baadhi ya hadithi katika diwani hii, kwa mfano katika hadithi ya 'Namchukia Babangu", maneno ya ushawishi ya Mafutu kwa babake Mzee Mkata M'mali kumsihi amnunulie baiskeli hata kama ni mkweche.Anamwomba:''Baba ama mie mwanao naumia, lakini naelewa, pia ulisoma kwa taabu, kila mara wewe hutuasa 'panda juani chumia kivulini'' mi...Naelewa lakini naumia, baba nakuomba uninunulie baiskeli, japo iwe mkweche, nitashukuru, Baba usinikatalie" Baba yake hakuitikia alimnyamazisha kwa kumwambia:'' ..Niondokee mvivu wewe!Kama umeyashiba masomo basi''(uk:112).

Dayalojia shawishi katika hadithi ya "Fimbo ya Maradhi' inadhirika pale ambapo Muthoni mkewe Thuo alipomshawishi mumewe wamfukuze mkaza mwana kutoka nyumbani mwao. Alimsihi mumewe:"Niliyoyajua hata kabla yake kuniarifu.Mwanamke huyo ashatuletea aibu katika mji huu. tutakuwa tunatembea nyuso tukiziinamisha kama kondoo.Bora Yule mwanamke sasa arudishwe kwao.'' Baada ya kuwaza alijibu:''leo siku yote nimeliwazia ulilonìachia. Mwanangu si busara kumrudisha Nyokabi kabla ya kudhibitisha madai unayohusishwa nayo.'' (uk:136).

Mzee Badi anatumia lugha ya ushawishi ili kumshawishi Shamsa akubali kuandamana naye kwenye chumba cha starehe ili waweze kubarizi kule.Mzee Badi anamrai ifuatavyo:
"Ndio ivyo kutoka leo" "Ah, nawe Shamsa! Tukapate hata gilasi ya maji tamu pale Royal Inn, kisha turudi kabla ya saa kumi," Badi akamlisha Shamsa nyama ya ulimi
Shamsha kwa wasiwasi alihoji:''Tutoke? twende wapi? (uk:151)

Juma ni mhusika anayetumia maneno ya ushawishi ili kuweza kumnasa Sista aliye mwizi wa simu katika hadithi ya'Sista Yule'. Anamshawishi mama mtoto aungane nao katika harakati na mipango ya kumnasa mwizi wa simu kwa kumwambia:
"Aisee ndiye huyo sista wetu", Juma alisema akipokea hela kutoka kwa yule mama mtoto. Hivi umeona jinsi alivyoitupia jicho simu ya huyu mama mtoto hapa?' "Hivi dada, unaweza kutuunga katika mpango wa kukomesha huu wizi wa simu kati ya hapa na sanawari?" Juma alimwuliza yule mama mtoto haraka haraka" Yule mama alijibu kwa mfadhaiko:'' Mbona ! Na miye hii ndio juzi tu nimeinunua!nimepoteza si chini ya simu sita!'' (uk: 20)

Maneno ya furaha ya kumtia moyo mhusika Lozi baada ya kupata mimba ni shawishi asiavye mimba aliyopata. Anamweleza kuwa kuteleza si kuanguka na ni hatua kubwa mbele, tena ya kasi, kwamba amzae mtoto na amlee:

"Lozi unajua kwamba hujafanya kosa lolote. Kutunga mimba ni tendo la kawaida tofauti ni kwamba umepata mimba wakati ambao hukuitarajia...kwa hivyo dada beba mimba yako, uzae na umlee mtoto wako" baada ya kutafakari Lozi alimjibu Furaha ifuatavyo:''Kweli wew ni zaidi ya rafiki...Kweli mimi ni mwanagenzi na kwa hakika nimekabiliwa na malimwengu ulimwenguni.'' (uk: 35).

### 4.1.2 Dayolojia Ulizi katika Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine

Hii ni dayolojia ambapo msemaji hutaka kujua zaidi, kudhibiti au kupata ushahidi. Katika diwani ya Alidhani Kapatana na Hadithi Nyingine, kuna dhihirisho ya mtindo huu katika hadithi mbalimbali. Dayolojia kati ya Nyaguthii na Beatrice katika hadithi ya 'Dakika za Adhama' chumbani walipolala na yule mwanaume baada ya kumwibia pesa inadhihirisha dayalojia ulizi: "Ni nani huyo?" Nyaguthii aliuliza. Ni mimi Beatrice,nifungulie tafadhali'' Beatrice akajibu. Wakati wa usiku wa manane huu? Lakini kumetendeka nini?" (uk: 68)

Pia mazungumzo baina ya Baba Sami na Mama Sami ni dhihirisho ya dayalojia ulizi ambapo mama Sami anataka kujua aendako Baba Sami:

"Safari ya wapi?"

Naenda kumuona daktari wa Sami............" (uk: 98). Pia mazungumzo baina ya Baba Sami na daktari ni dhihirisho ya kutaka kujua zaidi juu ya ni nani atakayempasha habari juu ya ungonjwa wa mwanawe Sami:

"Lakini habari hii tumfichulie nani? Twende tukitangaza mtaani kwamba mtoto wetu ameambukizwa ukimwi? Itatusaidiaje?

"Sio hivyo mzee" Daktari alieleza

"Ni vipi?' Baba Sami alihoji (uk:101)

Dayalojia ulizi kati ya polisi na Yakubu katika hadithi ya 'Baiskeli' inapelekea udadisi wa hali ya Yakubu na kuishia ndani ya seli: "Wewe ni mbwa? Ee. Sema haraka, wewe ni mbwa?" "....hawa ndio wanaouza bangi....au sio?" "Au utaongea vizuri, una chochote?"akauliza Mrefu . Askari mfupiu alifoka na kusema kwa ufidhuli '' haya , fuata sisi basi 'nyangau!' "' (uk:4)

Katika hadithi ya ''Sista Yule'' dayalojia ulizi inadhihirika wakati babu pale kwenye gari wanapanga njama ya kumkata Yule Sista ambaye alituhumiwa kwa wizi wa simu. Maswali yanayodadisi ili kupata ukweli yanatumika: "Hivi babu, huyo Sista huabiri gari wapi?" "Kweli yanawezekana? Mtu wa Mungu aibe? kwa nini? Tena Sista aliyevalia mavazi ya heshima na kujistahi?" "Sista? Sista maji ya kunde hivi? Kinywa kichafu sawa na maji taka? Fidhuli sawa na hawa utingo wa daladala?" (uk:13-14)

Maswali ya kutaka kujua zaidi juu ya hali ya Lozi pamoja na Furaha na Rhoda kama inavyodhihirika katika hadithi ya "Malimwengu" ni idhibati kuwa kuna matumizi ya dayalojia ulizi. Baada ya Lozi kurushwa nje ya nyumba na mkurugenzi Bwana Mark Pacha, Furaha anakuja kumfariji Rhoda wasaidiane. "Kufikia hapo, Rhoda alijipata kauli imemtimka "jamani kwema lakini?" Furaha akamjibu, kwema dada.' Rhoda hakuridhika na jawabu hilo, "Kumejiri nini?" Rhoda akahoji (uk:33)

Kutokana na ushahidi huu ni bayana kwamba Dioyolojia shawishi imedhihirisha ubanifu wa fani katika diwani ya '*Alidhani Kapata Hadithi Nyingine*'.

### 4.1.3 Dayolojia Malumbano katika Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine

Katika dayolojia hii mhusika hujibizana na mhusika mwenzake. Katika diwani ya 'Alidhani Kapata', matumizi ya dayalojia hii imedhihirika marakadhaa. Majibizano katika hadithi ya 'Bingwa kama Mimi' kati ya kisura Zuzu na Profesa inawatia moyo wanafunzi kujibidiisha, lakini bado hawaoni faida ya masomo, wana ubishi tu:

"Nini tena bibiye?"

"Lakini umesema tuipindue serikali'

"Nazungumzia mapinduzi ya kitamathali"

"Sikuelewi,"

"Basi njoo ofisini tuonane baada ya kipindi hiki ili nikufafanulie zaidi" (uk: 52)

Dayolojia malumbano imetumiwa na mwandishi katika hadithi ya 'Dakika za Adhama'. Mhusika Beatrice anapotorokea kwa Nyanguthii baada ya kumwibia yule mwenziwe mle chumbani. Beatrice anamdadisi Nyaguthii juu ya maisha yake na ubishi unazuka.

"Nataka kukuuliza swali moja tu Nyaguthii, kwa nini ulitoka kwenu?' Beatrice aliuliza

"Ni hadithi ndefu, Beatrice"

"Swali jingine moja, Nyaguthii si lazima unijibu, lakini nimekuwa nikihisi kuwa hunipendi na huwa unanidharau.''

"Sivyo. Beatrice sijawahi kukuchukia" (uk: 69)

Baina ya Baba Sami na daktari kuna malumbano. Wakati daktari anapomshauri Baba Sami juu ya afya ya mwanawe Sami, malumbano yalizuka. Dakitari alijaribu kumsaidia kwa kumpa ushauri:

"Sikiza mzee" alisema.

"Naam mwanangu. Enzi ya kuufichaficha ugonjwa huu ilipita kitambo."

"Lakini habari hii tumfichulie nani? Twende tukitangaza mtaani mtoto wetu ameambukizwa ukimwi? Itatusaidiaje?

"Sivyo mzee'

"Ni vipi?'(uk:100)

"Sioni kama Sami atakubali kujitangaza hadharani"

"Ni juu yako kama mzazi kumshawishi" (uk: 101)

Malumbano baina ya Mzee Mkata M'mali na mwanawe Mafutu, katika hadithi ya 'Namchukia Babangu' yanazua ubishi unaosababisha kifo cha Mafutu:

"....baba nakuomba uninunulie baiskeli, japo mkweche...Baba usinikatalie"

"Baba...baba usikatalie" "Baba ...baba, umeyasikia". Akataka kujua Mafutu

"Niondokee mvivu wee! Kama umeyashiba masomo basi!... Zatoka wapi fedha eti? Nikome!" "Nitakukoma baba, aushi daima"

Mifano hii ni baadhi ya ushahidi kuwa Dayolojia imedhihirishwa kwa ubanifu mkuu kwa sababu haijakuzwa katika utanzu huu wa hadithi fupi kama ilivyo katika utanzu wa tamthilia na riwaya.

## 4.2 MONOLOJIA

### Utangulizi

Wamitila (2008) anafasili uzungumzinafsia kwamba hutokea pale ambapo mhusika wa kidrama huzungumza pekee. Kimsingi ni kaida ya kidrama ambapo maneno yanayosemwa (au mawazo yanayowazwa) na mhusika akiwa pekee yake huchukuliwa kama nyenzo ya kuwepo kwa mawasiliano kati ya msomaji au mtazamaji kwa upande mmoja na mwandishi kwa upande wa pili.

Monolojia ni masimulizi katika kazi ya fasihi yanayofanywa na mtu mmoja tu. Mhusika anaweza kuzungumza peke yake. Mbatiah (2001) anaeleza kuwa uzungumzi nafsia ni hali ambapo mhusika anazungumza na nafsi yake au kutoa hotuba. Mbinu hii hutumiwa kuendelezea ploti na vile vile kukuzia maudhui kwa kubainisha mawazo ya wahusika.

Katika hadithi fupi monolojia ni dhana ambayo haitumiki sana kwa sababu wahusika hawakuzwi sana katika diwani hii, monolojia inadhihirika kwa kiwango fulani ili kukuza uhusika, maudhui na ploti. . Aina za monolojia ni kama vile: uzungumzaji kando,na uzungumzi nafsia. Tuna aina mbili za uzungumzi nafsia ambazo ni uzungumzi nafsia faragha na faraghuzi. Wasifu mwingine wa ubanifu wa fani katika '*Alidhani Kapata Na Hadithi Nyingine*' unadhihirika katika matumizi ya monolojia.

### 4.2.1 Monolojia katika '*Alidhani Kapata*'

Wamitila (2008) anasema kuwa mhusika anashiriki uzunguzi hapa husema mambo ya kibinafsi yanayomhusu na kwa njia hii hadhira inapata fursa ya kuyajua mawazo hayo ya kibinafsi.Tunaposhughulikia monolojia katika Alidhani Kapata na Hadithi nyingine tutaangazia: Jinsi monolojia ilivyojitokeza katika kazi hii. Waandishi mbalimbali wamekuza uzungumzi nafsia wa kifaragha katika usimulizi wao pekee ambapo hadhira tuli hupata nafasi ya kusikia hisia za ndani za mhusika. Mhusika mkuu Yakubu katika hadithi ya 'Baiskeli' anadhihirisha monolojia kupitia mawazo yake anapotoka nyumbani kuelekea kazini.

"Lakini haidhuru Mungu si Athumani. Jicho lake la ndani lilimwonyesha Yakubu kuwa ingefika siku ingawa hakujua lini ambapo angekuwa na kijibaiskeli chake. Hicho kingeweza kumfikisha hadi kazini mwake kwa haraka, starehe na bila uchovu" (uk. 1)

Bakari katika hadithi ya 'Sista yule' ana monolojia ya kimawazo. Anawaza jinsi ambavyo anaweza kuwakamata vibaka na wezi wa simu wa barabara ya Arusha kuelekea Moshi. Alikumbuka maneno na kauli ya yule mzee daladalani:

"Na hata hawa Masista wenye vinywa mwozo, moto wa jehanamu vilevile. "Kweli yawe yawezekana? Mtu wa Mungu aibe? Kwa nini? Tena sista aliyevalia mavazi ya heshima na kistaha? Lakini lisemwalo lipo, kama halipo basi lipo njiani laja." (uk :13)

Katika hadithi ya 'Malimwengu' mhusika Lozi anauzungumzi nafsia. Licha ya kuwa wanasafiri pamoja na Furaha na rafikiye, anazama kwenye mawazo mazito kwa sababu ya mimba aliyonayo. Ghafla akasikia sauti ikisema: "Usiniulie mjukuu wangu Lozi, usiniulie mjukuu wangu" Ilikuwa kama sauti kutoka kuzimuni. Lozi akagutuka na kutoa sauti, "Mama usiniache." (uk 34)

Mhusika Beatrice aliyefanya kazi katika baa alitamani kujitoa uhai kwa sababu ya kutopata mafanikio na upendeleo mahali pa kazi. "....ulifika wakati hata yeye Beatrice akatamani kwenda Metric "Lakini dhamiri yake ilimkataza. Alitamani mapenzi, alitamani kuishi" (uk 63)

Amiri ni mhusika katika hadithi ya 'Pendo la Siri', ambaye anajizungumzia kwa maneno na mawazo. Mrembo aliyemuona mle ukumbini mwa 'Taarab Night' alimbeba mzimamzima:

"Siku hiyo Amiri hakupesa jicho kwa jinsi alivyokuwa karowa kwa mahaba ya kisura wake wa 'Taarab Night'. Aliwasili kwenye akili yake, akaona wakikumbatiana na wakipokezana nyonda za hali ya juu" (uk124)

Monolojia ya mhusika Amiri katika hadithi ya 'Pendo La Siri' na ya 'Badi' katika 'Naye Huyo Mme Mwenzangu?' Inawasilisha maudhui ya mapenzi.Amiri anavutiwa na kisura wake wa 'Taarab Night': "Akili ilimtoa pale nyumbani ikampeleka ufukweni wakati wa maji mafu tena msimu wa kiangazi akawa amelala kwenye mchanga huku kisura huyo akimlalia kifuani akimwongoa kwa maneno ya mahaba. Alirejea ubeti wa wimbo wake mpya alioutunga kwa ajili ya mpenzi wake huyo aliyekuwa yeye Amiri akiumia kisirisiri kwa sababu yake." (uk:125)

"Audhubillabi" Amiri alitamka. 'Ya Rabbi niondoshee fikra za upotovu. Wala sitaki kutenda la haramu na huyo bibi. Akinikubali nitakwenda kwao nimpose nimwoe kihalali." (uk:126)

Mhusika Badi ana mapenzi kwa Saburi ambaye ni mfanyi biashara. Kiza inapokaribia kutawala, anamtegea Saburi kwa kijia na anajizungumzia. Anajiegemeza kwenye boneti la hilo 'surf'. Anatazama ujia wa miguu unaotokea madukani. "Vipi leo? Mbona haonekani? Si miye mwenyewe nimemwona pale dukani lake la urembo?" (uk:149)

Maudhui ya umasikini na chuki yadhihirika kupitia kwa monolojia katika hadithi ya "Namchukia Babangu". Mhusika Mtoro M'mali ametanguliza hadithi kwa maelezo ya kuwa anamchukia babake kuliko vyote katika dunia pevu. Umasikini waliotiwa na baba yao kama famila unamfanya yeye na ndugu zake kuwa na chuki dhidi ya babake:

"Na vipi nisikereke nijitazamapo nilivyo? Vipi nisiudhike nionapo dada zangu wawili walivyoteswa na dunia inayowakata mbele na nyuma mithili ya msumeno? Vipi nisiumwe nimkumbukapo marehemu kaka mafutu (uk: 110) .....tangu siku hiyo nikaapa kwamba daima shule ya upiliasilani nitaionapaa na ikatimu" (uk:113).

Maudhui pia ya umasikini katika hadithi ya Baiskeli yadhihirika kupitia kwa monolojia ya Yakubu. Yeye na familia yake waliishi katika umasikini uliokithiri, jambo linalomsababishia kuwaza na kuwa na shauku juu ya angalao kupata kijibaiskeli cha kumfikisha hadi kazini: "Lakini haidhuru, Mungu si adhumani. Jicho lake la ndani lilimwonyesha Yakubu kuwa ingefika siku –ingawa hakujua lini – ambapo angekuwa na kijibaiskeli chake. Hicho kingeweza kumfikisha hadi kazini mwake kwa haraka" (uk: 1)

Monolojia ya Njooki katika hadithi ya 'Fimbo ya Maradhi' inaashiria udhalilishaji na uonevu wa mwanamke wakati mkaza mwana Nyokabi aliwapasha habari juu ya ugonjwa wa Ndugire mumewe. Njooki alipofika na kuingia katika chumba cha mwanawe, alifoka:
"Njooki alisikika,"uu! ii! Mwanangu amelishwa sumu! Tulimjua mwanamke huyu, ukooo wao ni wa nasaba mbaya. Uuii! Ameniulia mtoto!" (uk:137)

Maneno ya uzungumzi nafsia ya Bakari katika hadithi ya 'Sista Yule' yanachangia pakubwa kuweza kuhakiki tabia na saikolojia ya mhusika huyu. Mawazo na mazungumzo yake yalikwamia tu kuwakamata wale vibaka na wezi wa simu wa barabara ya Arusha kuelekea Moshi. Kupitia kwa mikakati aliyoweka mwizi wa simu, Sista aliweza kushikwa. "Yaelekea huyo Sista alikuwa zaidi ya Sista. Mengi yanayohusu kupotea kwa simu, huenda kayapitisha yeye" (uk:13)

Monolojia ya Beatrice katika hadithi ya 'Dakika za Adhama', inatupa mwangaza juu ya mwenendo, mtazamo na tabia ya mhusika huyu. Maisha aliyopitia yalifanya moyo wake kuwa mgumu. Mazingira na hali aliyokuwa wakati huo yalimfanya kujihusisha na mambo yasiyostahili na kinyume na maadili kama vile ulevi, wizi na starehe potovu. "Alihisi

uchungu fulani ukimla ndani kwa ndani. Aliwaona wanaume wote kama watu waliokula njama ya kufanya maisha yake kuwa magumu.'' (uk: 68)

Mhusika Hamisi anashtuliwa na kifo cha dadake aliyemuenzi sana. Hamisi amekuzwa kutoka mwanzo wa hadithi hadi mwisho kama aliye na moyo uliojaa huruma na mapenzi kwa dadake hadi ugonjwa wa dadake unamfanya kuanguka mtihani wa chuo kikuu.

"Alihisi kuwa alizidi kuzama katika shimo la maisha. Alikukurika huku akipiga unyende, jambo lililozidi kumsikitisha ni kuwa dadake mpendwa masikini lazima katika ile ghari ghari ya mauti, alijaribu kutia maji ili ameze dawa" (uk: 79)

Uzungumzi nafsia wa Profesa Mkanawire Mkandawire katika hadithi ya 'Bingwa kama Mimi' unatoa mwanga juu ya tabia na saikolojia ya jinsi alivyokuwa kutoka mwanzo kama aliye na mwelekeo hasi na kuhusu vijana wasomi wa chuo kikuu. Mwelekeo wake kuwahusu ni kuwa wanapoteza muda wao bure:

"Visichana kama hivi ndivyo vinavyopoteza muda bure hapa chuoni. Usomi si milki ya kila mtu. Vinaharibu tu sura hapa. Afadhali vingetafuta wapiga picha wavipige picha na kuzianika kwenye majalada ya majarida ya urembo na mitindo ya mavazi." (uk: 45.)

**4.3 Hitimisho**

Dayalojia imekuzwa na kutumiwa na waandishi katika diwani ya 'Alidhani Kapata' na hadithi Nyingine kwa kiwango fulani. Waandishi wametumia aina mbalimbali za dayolojia, nazo ni pamoja na dayolojia shawishi, dayolojia ulizi na dayolojia malumbano. Dayalojia imedhihirika vizuri katika lughainayotumwa na wahusika kupitia jinsi wanavyosemezana. Lugha ya wahusika inawatambulisha wahusika wenyewe na kubainisha upekee wao. Pia maudhui mengineyo ya lugha yamedhiirika kupitia dayalojia

Waandishi wa diwani ya 'Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine' wamekuza monolojia ili kueleza na kujenga wahusika katika usawiri wao. Tumechanganua jinsi uzungumzi nafsia ulivyotumiwa na wahusika kuyaendeleza maudhui katika hadithi tofauti tofauti. Uhusika wao kuhusu maswala mbali mbali katika diwani *ya Alidhani Kapata na Hadithi Nyinginezo* na pia falsafa yao kuhusiana na hali tofauti katika hadithi mbalimbali umeshughulikiwa.

Kupitia kwa dayalojia na monolojia tunapata kuelewa mielekeo ya wahusika kuhusu wenzao. Kuwafafanua wahusika kwa kuibua tabia  na mielekeo na misimamo yao kuhusu mambo mbali mbali. Mbinu hizi zimetumika kwa ubanifu na vile vile zimesaidia mwandishi kubana maelezo yake kama ilivyodesturi katika utanzu huu.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi

Katika sura hii, tunawasilisha hitimisho la utafiti wetu. Sura hii ina sehemu zinazoshughulikia matokeo ya utafiti huu, umuhimu wa utafiti na mapendekezo ya utafiti zaidi juu ya diwani ya '*Alidhani kapata na Hadithi nyingine*'

### 5.1 Muhtasari

Imedhihirika katika utafiti huu kuwa si rahisi kuangazia au kuchanganua kipengele kimoja cha fani kwa upekee wake bila kuonyesha namna kipengee hicho cha fani kinahusiana na kingine katika kujenga kazi nzima. Uchunguzi huu umebaini kwamba wahusika wamesawiriwa kwa ubanifu wa upekee fulani ili kuwasilisha masuala mbalimbali katika jamii husika, masuala hayo ni pamoja na mapenzi, unafiki,matatizo ya asasi ya ndoa na maswala ibuka, kama: Mapenzi baina ya Shamsa na Badi, talaka baina ya Binta na Dennis kisha Dennis amuoa Sista Taziana.

Kuhusu mtindo wa waandishi katika diwani hii, tumegundua kuwa wametumia methali, semi na tamathali za usemi ili kuzua hisia na kusisitiza maana mbalimbali. Licha ya hayo, tumegundua kwamba methali, semi na tamathali za usemi zimechangia thamani ya kiujumi katika hadithi zilizomo katika diwani ya '*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*'. Tumebainisha pia kuwa tamathali za usemi zina umuhimu mkubwa kwa vile zimetumiwa kufafanua maana, kutoa mifano mwafaka, kuibua hisia, kuzua ucheshi mbali na kuongeza ujumi wa kisanaa. Kwa hivyo madhumuni ya utafiti ya kubainisha jinsi ubanifu wa matumizi ya lugha ulivyochangia utafiti wetu na kuendeleza maudhui na dhamira imetimia vyema, na

pia kujibu swali la utafiti wetu la je, ubanifu wa matumizi ya lugha una nafasi gani katika kuendeleza maudhui na dhamira ya waandishi mbalimbali katika diwani hii?

Katika uchunguzi wetu tumebainisha kwamba wahusika wakuu katika hadithi tulizochanganua ni wahusika wa mraba mmoja kwa sababu hawabadiliki licha ya hali na mazingira kubadilika na walidhihirisha ubanifu wa kifani katika uwasilishaji wao. Hali hii ni tofauti na katika riwaya ambapo wahusika wakuu huwa wa kimviringo. Ni bayana kwamba wahusika wa hadithi fupi hawakuzwi sana kama ilivyo katika tanzu zingine kama vile riwaya. Pia tumegundua kuwa mwandishi wa hadithi fupi humulika na kushughulikia swala moja, hivyo, kuhalalisha vitambulishi vya kimaudhui na kifani za hadithi fupi.

Katika kiwango cha matumizi ya lugha katika diwani ya '*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine'* uchanganuzi wetu umeangazia methali, semi na tamathali za usemi huku tukijibu swali la utafiti: Je, matumizi ya lugha una nafasi gani katika kuendeleza maudhui na dhamira katika diwani ya *'Alidhani Kapata na Hadithi* Nyingine'?.

Tumengudua kwamba waandisdhi wa hadithi tofauti wamekuwa na uhuru wa kutumia methali, semi na tamathali za usemi kwa kusudi la kuwasilisha mawazo yao na kuacha athari fulani waliyoinuia. Uhuru huu umechangia sana katika uchanganuzi wetu wa matumizi ya lugha. Pia tumebaini kuwa waandishi wametumia methali, semi na tamathali za usemi zilizofungamana na matukio, muktadha na mazingira ya hadithi fupi husika. Fauka ya hayo, tumebaini kwamba waandishi wametumia sentensi anuwai katika uandishi wao. Wamechanganya matumizi ya sentensi fupifupi na ndefu. Ni wazi kuwa sentensi fupi ni maarufu katika utanzu huu lakini muktadha huwafanya waandishi kutumia sentensi ndefu inapohitajika.

Pia tumengudua kuwa matumizi ya dayolojia na monolojia katika hadithi fupi yamechangia katika kuzua hisia, kuibua na kuendeleza maudhui. Kutokana na matumizi ya dayolojia tumeweza kubaini aina za dayolojia zilizotumika nazo ni; dayolojia shawishi, dayolojia ulizi na dayolia malumbano ambazo zimechangia kuisukuma hadithi mbele.

Nadharia ya elimu – mitinda imetufaa sana katika usawiri wa wahusika katika '*Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*' nadharia hii imetusaindia kuona utenzi wa waandishi kuhusu usawiri wa wahusika.

Kuhusu umuhimu wa utafiti wetu, tumethibitisha kuwa fani na mtindo katika utanzu wa hadithi fupi haujashughulikwa sana ikilinganishwa na tanzu zingine za fasihi andishi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu utanzu huu umepuuzwa na umechukuliwa kama utanzu usio na uzito kama riwaya, tamthilia na ushairi kwa hivyo basi, utafiti huu umetoa mwanga wa kuhakiki fani na matumizi ya lugha katika utanzu huu na kuongezea mchango wa kuhakiki katika utanzu huu.

### 5.2 Mapendekezo ya utafiti zaidi

Katika utafiti huu tumeshughulikia vipengele vinne vya ubanifu wa fani ambavyo ni wahusika, dayolojia, monolojia na matumizi ya lugha. Kuna vipengele vingine vya fani kama vile muundo, mandhari na mtindo. Kwa hivyo, kuna haja ya kutafitia vipengele hivi katika diwani ya '*Alidhani Kapata na_Hadithi Nyingine*" na kuonyesha ufaafu wake.

## MAREJELEO


Culler, J. D. (1975). *Structurist Poetics*. London. Routledge and Kegan Paul.

Fokkema, D. W. (1997). *Theories of Literature in the 20th century*. London. C. Hurst and Company.

Habwe, J. na Karanja, P. (2005). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi. Phoenix Publishers.

Indagasi, H. (1988). Stylistics. Nairobi University Press.

Iribemwangi, P. I. (2011). *Alidhani Kapata na Hadithi Nyingine*. East African Education Publishers ltd. Nairobi. Kenya.

Kimani N., Rocha C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi. Kenya.

Leech, G. na Short, M (1981). *Style in fiction: A linguistic introduction to English fictional prose*. Newyork: Longman Group Ltd.

Massamba, D. et al. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Sekondari na Vyuo. Dar-es - Salaam. TUKI.

Mc Onyango, O. (Mh) (2008). *Mimba Ingali Mimba na Hadithi Nyingine*. Focus publishers. Nairobi. Kenya.

Mbatiah, M. (Mh) (2010). *Mwendawazimu na Hadithi Nyingine*. Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi. Kenya.

---------------------------- (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi. Standard text books graphic and Publishing

Mbuthia, E. M. (2005). *A stylistic and Thematic Analysis of Kiswahili Short Stories"*. Tasnifu ya Ph.D Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mohamed, S. A. (1995). *Kunga za Nadhari ya Kiswahili*. East African Educational Publishers: Nairobi.

Mohochi, E. (1995). *"Fani katika Hadithi fupi za Kiswahili"* Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Egerton. (Haijachapishwa)

Msokile. M. (1993). *Misingi ya hadithi fupi*. Dar-es-salaam University press.

Mwangi, (2005). *"Uhakiki wa Fani katika tamthilia za K.W. Wamitila*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Musyoka, (1996). *"Uhakiki wa Fani katika tamthilia za jay Kitsao*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Poe, E. A. (1938). *The Complete Tales and Poems*. New York. Random House.

Scholes, (1974). *Structurism in literature*. New Haven. Yale University.

Wafula, (1999). "*Uhakiki wa Tamthilia. Historia na Maendeleo yake*. Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula R. M. na Kimani, N. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi. Kenya.

Wales K. (2001). *A Dictionary of Stylistics (*2nd Edition). England; Pearson Education Ltd

Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya fasihi*. Vide-muwa publishers limited. Nairobi Kenya.

---------------------- (2007) *Lulu za lugha. Kamusi ya tashibihi, vitendawili, milio na mishangao*. Nairobi; Loghorn publishers

--------------------- (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Focus publications. Nairobi. Kenya.

--------------------- (2003). *Kichocheo cha fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Books.

--------------------- (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publishers Ltd. Nairobi.

--------------------- (2001). *Kamusi ya methali*. Nairobi: Longhorn publishers.

--------------------- (1999). *Kamusi ya misemo na Nahau*: Nairobi: Longhorn Publishers.